Jumanne Novemba 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581858 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 2

**Hoja** ya Tundu Lissu yaibua mvutano mahakamani



UKURASA 3

**Tujilane** Chizumila; kutoka kuwa binti mkimbizi hadi jaji wa mahakama kimataifa



UKURASA 5

**CCM** tumewekewa mapingamizi na tunaamini haki imetendeka - Makalla

## TAKUKURU YABAINI...

# 'Chawa' watumika kupenyeza rushwa

• **Lengo** wagombea wajitoe Uchaguzi wa Mitaa; wapigakura nao waandaliwa 'asante' yao... *Endelea ukurasa 2*

# Wakulima warejeshewa mifuko ya viuatilifu vya korosho iliyofanyiwa mchezo mchafu

UKURASA 7




Skani hapa kutembelea chaneli yetu



Miundombinu ya SGR

# Wanaswa na shaba zinazodaiwa za SGR

UK. 3

**MICHEZO** BODI YA LIGI YAIJADILI YANGA KUHAMIA KMC UK.24

**MAONI,** UK.6



Katibu wa Bunge la Tanzania, Baraka Leonard (kushoto) akishikana mkono na Naibu Katibu wa Bunge la Kenya, Jeremiah Ndombi mara baada ya kukabidhi nafasi ya Mwenyekiti wa Mkutano wa Makatibu wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Bunge la Kenya. Makabidhiano hayo yamefanyika katika Mkutano wa Makatibu uliofanyika Nairobi Kenya jana. **PICHA: BUNGE**

# TAKUKURU: Vigogo wanatumia 'chawa' kupenyeza rushwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani hapa, imebaini baadhi ya viongozi kisiasa wanafadhili vitendo vya rushwa katika mchakato wa uchaguzi unaoendelea, ili kubadili utashi wa baadhi ya wagombea na wapigakura.

Kwa mujibu wa TAKUKURU, mbinu zinazotumika ni kuhonga baadhi ya wagombea wajitoe, ama wajaze fomu vibaya au kuchelewesha kuzirejesha kwa ajili ya uteuzi, wahongaji wakidaiwa kujenga mazingira ya kupita bila kupingwa.

Mkuu wa TAKUKURU Kahama, Abdallah Urari aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa 'vigogo' hao wameunda vikundi vya vijana wafuasi wao, maarufu chawa', wanaowatumia kusambaza fedha kwa walengwa na kuendesha ushawishi wa kufanikisha malengo yao kwa wagombea na baadhi ya wapigakura.

Urari alikuwa anafafanua kuhusu hali ya rushwa na wajibu wa vyombo vya habari katika mapambano hayo kipindi hiki cha mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Alisema kuwa baadhi ya viongozi wamekuwa na tabia ya kuunda makundi maalumu ya vijana aliowaita 'chawa', ambao wanawatumia kugawa rushwa kipindi cha uchaguzi.

Kiongozi huyo alisema kuwa hivi sasa wanawafanyia sherehe mbalimbali kila siku, hata kuwasafarisha kuzuru kaburi la Baba wa Taifa na kuwapeleka kutembea mbuga za wanyama.

Urari alisema wamebaini kuwa vijana hao pia wanaahidiwa kupatiwa nyadhifa za uongozi watakapokamilisha kazi waliyopewa.

"Vijana hao wamekuwa wakiwahadaa wananchi kwa kuwapatia Sh. 5,000, hali ambayo ni hatari, kutapatikana viongozi wasiofaa na wananchi kukosa viongozi wanaowahitaji.

"Watapata (viongozi) ambao hawawezi kuwaletea maendeleo, hivyo niwatake kuacha mara moja vitendo hivyo kwani vinachafua taswira ya nchi.

"Hawa vijana wanaandaliwa kwa majina mbalimbali, ikiwamo 'Timu Kazi' na kuwatumia kugawa rushwa. Kwa sasa tunajipanga kuwachukulia hatua kali za kisheria kwani hatupo tayari kuvurugwa kwa uchaguzi. Tutaanza tutatoa elimu kwa vyama vya kisiasa kabla ya kuanza kuwachukulia hatua," alisisitiza Urari.

Ofisa Uchunguzi wa TAKUKURU Wilaya ya Kahama, Mlamuzi Kuhanda alisema wamebaini baadhi ya viongozi ambao wamekuwa wakiwapatia rushwa wagombea ili wajiondoe katika uchaguzi.

Alisema wamekuwa wakiwataka kujaza fomu vibaya, kutokurudisha fomu kwa wakati au kurejesha fomu muda ukiwa umekwisha ili wapite bila kupingwa.

Aliwasisitiza viongozi kuacha mara moja tabia hiyo kwa kuwa inasababisha kuwa na viongozi ambao siyo hitaji la wananchi na wale watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani; mtoa rushwa na mpokeaji, wote wana makosa kwa mujibu wa sheria.

Mkazi wa Mhongolo, Manispaa ya Kahama, Williamu Bundala alidai kushuhudia "vikundi vya vijana wa viongozi" na wamekuwa wakisumbua mitaani kuwashawishi kuwachagua baadhi ya viongozi.

Bundala pia alidai vijana hao wamekuwa na shughuli za sherehe nyingi kila kukicha na hata kutembelea mbuga za wanyamapori.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# Hoja ya Lissu yaibua mvutano mahakamani

**Na Elisante John,** SINGIDA

KESI ya Uchochezi inayomkabili Askofu Machumu Kadutu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima la jijini Dar es Salaam, aliyeshitakiwa mkoani Singida, imechukua sura mpya, baada ya Wakili Tundu Antipas Lissu kuomba mahakama itupilie mbali shauri hilo, akidai mashtaka hayana mashiko.

Katika shauri hilo la jinai namba 19525 la mwaka 2024, Askofu Kadutu ameshtakiwa kwa kutamka maneno yanayodaiwa ya uchochezi wakati akihutubia mkutano wa hadhara wa siasa.

Wakati wa mkutano huo wa siasa uliofanyika Juni 3 mwaka huu katika kijiji na kata ya Ibaga, wilayani Mkalama, mkoani Singida, ilidaiwa mahakamani na Wakili wa Serikali Almachius Bagenda kiongozi huyo wa kiroho alitenda kosa linaloweza kujenga chuki kwa wananchi dhidi ya askari na serikali yao kutokana na uchochezi.

Wakili Bagenda alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mfawidhi wa mahakama hiyo kuwa, siku ya tukio, Askofu Kadutu alitamka maneno kuwa, "...naweza kukosea njia wakati wa kwenda lakini huwezi kukosea njia wakati wa kurudi, mmeshaifahamu njia.

"Walichofanya 2019 hakitajirudia... wangapi nyumbani mna majembe, wangapi mna visu nyumbani, wangapi nyumbani mna panga... ? Sasa mimi ninawaambia hivi kama kupitia polisi... kama wamerudia tena katika uchaguzi ili wapitishe wanavyotaka wao, haki ya Mungu safari hii haya majembe yatakuwa na matumizi mengine... wakiwa nanii na nyie mnafanyaje? Mnawananiii..."

Wakili Bagenda alidai maneno hayo aliyoyasema katika eneo la soko la zamani eneo la Madukani kwenye kijiji cha Ibaga, ni ya uchochezi na kinyume cha sheria.

Baada ya maelezo hayo, Wakili Lissu aliimwomba Hakimu Mkazi Mkuu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida, Allu Nzowa kupitia shauri dogo alilolifungua mahakamani hapo, atupilie mbali shauri hilo, hoja iliyoibua mvutano wa kisheria, Wakili wa Serikali Bagenda akiipinga.

Hata hivyo, Hakimu Nzowa ilibidi aahirishe mahakama kwa muda wa nusu saa kutoa nafasi kwa pande zote kupitia vifungu vya sheria kabla ya kurejea tena kuendelea na mahakama.

Baada ya kurejea, upande wa serikali ilijibu hoja za Lissu, huku Lissu naye akiwa na hoja zake za kisheria. Hakimu Nzowa akaahirisha shauri hilo hadi Desemba 2 mwaka huu, atakapotoa uamuzi juu ya pingamizi lililowekwa na upande wa utetezi, unaodai shauri hilo halipaswi kuendelea kusikilizwa mahakamani.

Jopo la Mawakili wa Serikali liliongozwa na Bagenda, aliyesaidiwa na Nehemia Kilimhana na Michael Martin, huku Lissu akisaidiwa na Hemedi Kulungu.



**HABARI KITAIFA**

# Wanaswa na shaba zinazodaiwa za SGR

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma linawashikilia watu sita kwa tuhuma za kuharibu na kuiba nyaya za shaba katika mradi wa reli ya kisasa (SGR) maeneo ya wilaya za Mpwapwa na Bahi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alisema kuwa katika wilaya ya Mpwapwa, jeshi hilo linawashikilia watu wawili; Said Sempinga (39) na Michael Robert (44), wote wakazi wa Kilosa kwa tuhuma za kuharibu miundombinu hiyo ya SGR.




Alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 3 mwaka huu saa tano usiku katika kijiji cha Msagali, wilayani Mpwapwa ambako watuhumiwa wanadaiwa kukata na kuiba nyaya kwenye madaraja matatu ya reli hiyo.

"Kufuatia tukio hilo jeshi la polisi lilipata taarifa na kuanza uchunguzi wa tukio hilo mara moja kwa kushirikiana na wananchi na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao kwa nyakati tofauti wakiwa na nyaya hizo walizoiba kutoka kwenye reli ya umeme, uchunguzi unakamilishwa ili hatua zingine za kisheria zifuate," alisema.

Kamanda Katabazi alisema katika tukio lingine lililotokea Oktoba 8 mwaka huu maeneo ya Bahi sokoni, wilayani Bahi, walikamatwa watuhumiwa wanne kwa nyakati tofauti kwa tuhuma za kuhujumu miundombinu hiyo.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Said Kapambwe (38), Petro Yassi (22), Michael Leyaseki (27) na Issa Misami (42).

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na polisi kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu wanaohujumu miundombinu hiyo kwa kuwa wanaliingizia taifa hasara kubwa.

# Kutoka mkimbizi hadi kuwa Jaji

## ●Akumbuka aliyemhukumu kunyongwa kuruka kizimba na kukimbia

**Na Christina Mwakangale**

JAJI Tujilane Chizumila (71), alikuwa na umri wa miaka 12 wakati alipoingia nchini Tanzania akiwa na wazazi wake kama wakimbizi, wakitokea nchini Malawi.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti hili juzi, jijini Dar es Salaam, amesimulia masuala mbalimbali ya jinsia, diplomasia, sheria na hadhi ya ukimbizi iliyomwachia alama maishani.

Kwa sasa ni miongoni mwa majaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, yenye makao yake makuu jijini Arusha.

Anasimulia safari yake tangu akiwa mtoto hadi kushika nyadhifa tofauti ikiwamo ubalozi nchi tofauti barani Afrika.

"Nilikuwa mtoto mkimbizi tangu nikiwa na miaka 12 hapa Tanzania, nilikuja na wazazi wangu na baba yangu alikuwa ni mwana-siasa. Tulipopata tu uhuru mwaka 1964, Malawi, akachaguliwa kwenda UN (Umoja wa Mataifa) kuiwakilisha nchi.

Baada ya mwaka mmoja ikatokea vurugu kati ya mawaziri na Rais Banda (Kamuzu), hii ikaathiri watu wote ambao walikuwa marafiki zake waliosoma pamoja, kufanya kazi pamoja, akaitwa arudi (Malawi).

Lakini baba akapigiwa simu na marafiki zake kwamba asirudi, kwa sababu kulikwisha andaliwa magari mawili ya polisi, moja sisi na mama na lingine kumbeba baba yangu kwenda kumfunga," anasimulia Jaji Chizumila.

Hali hiyo ilimfanya baba yake na familia yake atoroke kutoka UN alikokuwa anaiwakilisha nchi yake kuja kuwa wakimbizi Tanzania.

"Nimeishi hapa kwa miaka mingi, nimesoma hapa. Niliolewa hapa, lakini baadaye nilitengana na mume wangu na kurudi Malawi."

Niliporudi Malawi niliendelea na kazi nyingine ikiwamo ya jaji na kuajiriwa Mahakama Kuu ya nchini humo.

Kwa sasa nimeajiriwa katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, najivunia, naishukuru Serikali ya Tanzania na UNHCR (Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Wakimbizi)," anasema.

Jaji Chizumila ameandika kitabu chenye jina: 'From A Refugee Girl to A Judge: My Journey', kinachosimulia maisha ya kuwa na hadhi ya ukimbizi pamoja na umuhimu na msaada kupewa kundi la aina hiyo, wanapofikwa na hitaji hilo.

"Kuwa mwanasheria haikuwa ndoto yangu bali baba, kwanza alitaka nisomee elimu niwe mwalimu na chaguo la pili liwe sheria. Ila binafsi nilipenda kuwa mwongoza ndege ambao hukaa kufuatilia mawasiliano katika chumba maalumu kabla ya ndege kupaa na kutua.

Lakini kwa sasa mimi kuwa katika chombo cha kisheria na haki za binadamu ni sehemu ya kurejesha fadhila kwa kile nilichofanyiwa na UNHCR na nchi (Tanzania) kunipokea na familia yangu kwa ukarimu hadi kufikia hapa nilipo," anasema Jaji Chizumila.

Miongoni kesi zilizomwachia kumbukumbu ni aliyoiendesha na kutoa hukumu nchini Malawi, akiwa Jaji, baada ya mtuhumiwa wa mauaji kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa na kuamua kuruka kutoka kizimba cha mahakama na kutoroka.

"Nakumbuka nikiwa jaji wa Mahakama Kuu ya Malawi, kulikuwa na kesi ya mauaji, mwanaume alikwenda kuiba mbuzi kwa jirani, halafu jirani alikuwa ni mtu mzima, aliposikia mbuzi wanalia alimkuta huyo mtu, akamtambua ni jirani yake.

Yule mtuhumiwa aliamua kumuua mwenye mbuzi wake na mbuzi aliowaiba aliwachinja na kuanza kuuza nyama.

Watu kijijini walianza kujiuliza yule mtu hakuwa mfugaji, ile nyama aliipata wapi? Kesi hiyo ikanifikia Mahakama Kuu, akawa anajitetea kwamba anaonewa. Ushahidi ulikuwa wazi, aliiba na aliua na kati ya ushahidi, mmoja ulionesha ngozi ya mbuzi ilikuwa ni ya 'brown', na kijiji chote mbuzi rangi hiyo alikuwa ni wa yule aliyeuawa.

"Ndani ya mahakama nikamwambia onesha rangi ya 'brown' humu mahakamani kama unaona, akaenda akashika benchi la 'brown' rangi ya mbao mninga iliyoiva, alijuaje brown? Wazee wa Mahakama ambao awali walisema hana hatia, wakatazamana. Wakakubali alitenda kosa.

Mtuhumiwa aliamua kuruka kwenye kizimba na kuanza kukimbia kwenda nje ya mahakama, lakini akakamatwa, iliniogopesha. Angeweza kufanya chochote kwangu, watu hudhani jaji ndio huamua kila kitu, kumbe tunashirikiana katika kuamua."

Usikose simulizi zaidi za Jaji Chizumila, kwenye makala wiki hii, kuhusu kuukataa ubaguzi wa rangi hadi sasa anavalia mavazi ya asili pekee ya kiafrika, isipokuwa awapo mahakamani tu.


**CANCELLATION AND RE-ADVERTIMENT FOR TENDERS**

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

**01. Cancellation of Tender No. TTU/T/G/01/2024/2025**
**A tender No. TTU/T/G/01/2024/2025 has been cancelled on November 12, 2024.**
**02. Re- advertisement of tender No. TTU/T/G/01/2024/2025**
for
Supply of T-shirts and Caps

**November 12, 2024**

1. This Invitation for Tenders follows Tanzania Teachers' Union, which appeared in Tanzania Teachers' Union financial regulations 3rd Edition of 2018.
2. Tanzania Teachers' Union has set aside funds for the supply of T-shirts and Caps during the financial year **2024/2025**.
3. Tanzania Teachers' Union now invites tenders from eligible Supplier to Supply T-shirts and Caps.
4. Tendering will be conducted through Competitive Tendering method specified in Tanzania Teachers' Union Financial Regulations 3rd edition of 2018.
5. Interested eligible Tenderers may obtain tender document physically at Tanzania Teachers' Union, and pay tender participation of non-refundablefee of Tanzania Shillings 500,000. Payment is performed through bank via account National Microfinance Bank(NMB) 20101300312 Name Tanzania Teachers' Union and collect set of Tendering Documents physically at Tanzania Teachers' Union Head quarter office, Jamhuri Stadium from 9:00 AM to 03:00 PM (Monday to Friday).
6. All Tenders must be physically submitted in the proper format, at or before 26/11/2024, 10:00AM. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend at TTU- Head quarter office, ground floor meeting room, Box 3077, Jamhuri Stadium Dodoma.

General Secretary - TTU
**Tanzania Teachers' Union –TTU**
**P.O.BOX 3077**
**DODOMA**

KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

# The Guardian, TMF wazindua dawati la TIJA

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya The Guardian Ltd inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian, kwa kushirikiana na Tanzania Media Foundation (TMF), imezindua dawati la uandishi wa habari wa tija kwa lengo la kuboresha maudhui yake.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa dawati hilo, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya The Guardian Ltd, Jackson Paulo, alisema anaamini mradi huo utakuwa na matokeo mazuri.

Alisema mradi huo utaanza Novemba 18 mwaka huu na utafanyika kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Ni mradi ambao ukiuangalia unaona kabisa umezingatia weledi na ambao unaona mwisho wa siku utaleta matokeo mazuri siyo tu kwa waandishi wa habari, bali pia kwa kampuni na umma.

"Kwa hiyo, sisi (The Guardian Ltd) tumeupokea, tutasapoti kwa mikono miwili na tunategemea tutaongeza ile asilimia ya uandishi wa habari wa tija kwa kiwango cha kutosha. Matamanio yangu ni angalau kwa mwaka wa kwanza, uandishi wa habari wa tija utaongezeka na tutakuwa na habari nyingi za aina hiyo (za maslahi ya umma)," alisema.

Kiongozi huyo wa The Guardian Ltd, alisema mradi huo unakwenda sambamba na kaulimbiu ya kampuni hiyo ya kuamini kwenye kitu kizuri ambacho hakipatikani mahali pengine isipokuwa katika kampuni hiyo.

"Falsafa yetu hapa ndani tunaamini katika 'high value content' (maudhui yenye thamani kubwa), ambayo haiko kila mahali... Kwa hiyo, lengo lenu (TMF) linaendana na sera yetu, hivyo tumekutana," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TMF, Danstan Kamanzi, alisema dawati hilo litahusisha waandishi wa habari, wahariri wabobevu, wataalamu wa sekta (eneo) husika na wanasheria, hivyo waandishi wataandaa na kuchapisha habari zinazohusu masuala mahsusi ikiwamo elimu, afya, kilimo, mazingira, siasa na mengineyo, yaliyofanyiwa uchunguzi wa kina ili kuleta matokeo chanya kwa jamii.

Kamanzi alisema TMF inaamini katika kuwajengea uwezo waandishi wa habari na kwamba wakati wote wamekuwa wanasisitiza uandishi wa habari wa tija ambao ndio wenye manufaa kwa umma.

Ni uandishi ambao Kamanzi alisema unafanyika kwa kiwango cha chini nchini. Akirejea utafiti wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wa mwaka 2022, Kamanzi alisema maudhui ya vyombo vya habari nchini yanaonesha uandishi wa aina hiyo unafanyika kwa asilimia nne tu nchini.

Alisema uandishi unaofanywa kwenye vyombo vya habari nchini, haujafikia viwango vizuri kwenye eneo hilo la uandishi wa habari wa tija (habari zinazojikita katika kumulika uwajibikaji na maslahi ya umma).

Kamanzi alisema utafiti huo wa SJMC unaonesha ubora wa maudhui ya vyombo vya habari nchini kwa mwaka 2018 ulikuwa ni asilimia 27, mwaka 2021 ulikuwa asilimia 22 na mwaka 2022 ulikuwa wa asilimia 30.



Dastan Kamanzi Mkurugenzi Mtendaji wa TMF akimwonesha Naibu Meneja Mkuu wa kampuni ya The Guardian Ltd, Jackson Lema muundo wa dawati la Tija (Tija Desk) lililozinduliwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania, EU kuimarisha ushirikiano

**Na Joseph Mahumi**

TANZANIA imeshukuru Umoja wa Ulaya (EU) kwa kuendelea kuwa miongoni mwa washirika wakubwa wa kimkakati wa maendeleo nchini katika kuisaidia masuala ya bajeti na sekta muhimu licha ya ukweli kwamba baadhi ya washirika wa maendeleo walijiondoa.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu El-maamry Mwamba, wakati akifungua kikao cha majadiliano kwa ajili ya kusaidia bajeti ya Serikali ya Tanzania jijini Dar es Salaam, kikijumuisha wataalamu kutoka Serikali ya Tanzania na EU.

Dk. Mwamba alisema serikali inatambua mchango mkubwa wa EU katika kuchangia maendeleo ya nchi ambapo kwa mwaka wa fedha uliopita (2023/24), walisaidia Euro milioni 40.819 kwa ajili ya kuongeza nguvu katika sekta za nishati, uchumi wa buluu, digitali, usawa wa kijinsia na Mradi wa Green and Smart Cities.

"Tumeshuhudia maendeleo ya makubwa na mazuri chini ya programu hii kutoka katika mtazamo wa sera hadi mafanikio halisi ikiwamo kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mpango wa Corporate Plan-6 na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha katika mtazamo wa sera," alisema.

Dk. Mwamba aliongeza kuwa upande wa utendaji, msaada mkubwa umekuwapo katika kukamilisha Mfumo wa Kitaifa wa Kutoa Hati Fungani za Kijani (Green Bonds), kuanzishwa kwa Mfuko wa Kitaifa wa Uwekezaji wa Mitaji, kupungua kwa asilimia ya kadirio la kodi, kuongezeka kwa usajili wa walipakodi na ongezeko la mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (MSME) kati ya jumla ya mikopo inayotolewa na benki na taasisi ndogo za fedha nchini.

Mkuu wa Masuala ya Ushirikiano wa EU, Marc Stalmans, alishukuru Tanzania kwa kuendelea kuwa mdau mzuri wa umoja huo na msimamizi mzuri wa shughuli zake ambazo zina manufaa kwa wananchi wake.

# Biteko awataka wana CCM kuepuka makundi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuepuka makundi ili kupata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu, 2025.

Alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wana CCM, kwenye Mkutano Mkuu wa CCM, Jimbo la Dodoma mjini.

Alisema kama CCM inahitaji ushindi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025, wanachama wanapaswa kuvunja makundi yao na kuwa kitu kimoja kukipigania chama.

"Kama tunahitaji kushinda ni lazima kuwa kitu kimoja kufanya kazi kwa ushirikiano tutofautiane katika vikao vyetu vya ndani, lakini tukitoka nje tuwe kitu kimoja kwa ajili kukipigania chama chetu kushinda kwenye chaguzi hizo," alisema Dk. Biteko.

Aidha, alisema ana imani kuwa CCM itafanya vizuri kwenye chaguzi zote hizo kutokana na maandalizi yanayoendelea kufanyika ndani ya chama.

"Sioni kama kuna chama kingine ambacho kimejiandaa kama ilivyo kwa CCM, lakini pia licha ya maandalizi hayo pia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi uliofanywa na chama chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM, Dk. Samia Suluhu Hassan, vinatosha kabisa kukipa ushindi wa kishindo chama chetu," alisema.

Kuhusu changamoto zilizopo kwenye Jimbo la Dodoma mjini, ikiwamo kukithiri kwa migogoro ya ardhi Dk. Biteko aliziagiza mamlaka zinazo husika kuipatia majibu ili wananchi wapate haki yao.

"Kuhusu migogoro ya ardhi katika jiji la Dodoma kama ilivyo elezwa awali na Mbunge Mavunde, niwaombe viongozi wa serikali hasa wale waliopo katika wizara husika kupatia ufumbuzi ili wananchi wapate haki yao na kwa wakati," alisema.

Vilevile, kuhusu uhaba wa maji katika Jiji la Dodoma Dk. Biteko alisema Wizara ya Maji inapaswa kutekeleza maagizo ya Rais ya kuchimba visima virefu ili wananchi wapate huduma ya maji ya uhakika wakati wakisubiri miradi mikubwa ikamilike.

"Wakati tunasubiri miradi mikubwa ya bwawa la Farkwa pamoja na kutoa maji katika Ziwa Victoria, tunapaswa kuendelea kuchimba visima virefu ili kukabilina na tatizo la uhaba wa maji katika jiji la Dodoma," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika jimbo la Dodoma kwa kipindi cha miaka minne Mbunge wa Antony Mavunde, alisema pamoja na mafanikio yaliyopatika, bado zipo changamoto kadhaa.

"Kutokana na serikali kuhamia Dodoma mahitaji ya maji yameongezeka na kusababisha mgao wa maji kwani hivi sasa mahitaji ya maji ni lita milioni 147 kwa siku na uzalishaji ni lita milioni 97 hivyo kufanya upungufu kuwa ni lita milioni 68 kwa siku," alisema Mavunde.

Pia, alisema katika kipindi cha miaka minne wamepokea fedha Sh. trilioni 1.5 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika jimbo la Dodoma Mjini.

Alisema fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa uwanja wa ndege Msalato, barabarani ya mzunguko kilomita 112.3, ujenzi wa uwanja wa maonyesho ya NaneNane ya kudumu na mji wa serikali Mtumba.

Alitaja miradi mingine kuwa ni ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu, chuo cha ufundi, soko la kisasa la Machinga, hospitali, vituo vya afya na zahanati, shule za sekondari na msingi na miradi ya maji.

Katibu wa CCM, Mkoa wa Dodoma, Pili Mbanga, alisema wanaendelea na maandalizi mbalimbali ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika uchaguzi wa serikali za mitaa, mwaka huu.

Alisema jumla ya wanachama 17,657 wameteuliwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unatarajiwa kufanyika Novemba 27,2024.

# ACT, CHADEMA wadai kuchoshwa wagombea wao kuenguliwa

**Na Elizabeth Zaya**

VYAMA vya ACT-Wazalendo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), vimedai kuchoshwa na kutoridhishwa na kinachoendelea katika hatua ya sasa ya uteuzi wa wagombea kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, viongozi wa vyama hivyo walisema hatua inayoendelea sasa inawafikirisha na kukosa uvumilivu, wakifikiria kujipanga kwa uamuzi mwingine endapo wagombea wao hawatarejeshwa katika kinyang'anyiro hicho.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema wagombea wao wengi waliokuwa wameteuliwa wameendelea kuenguliwa na hawafahamu kama kuna watakaobaki kutokana na kazi hiyo ya kuengua inayoendelea nchi nzima.

"Kama mnakumbuka, tangu tarehe nane, wagombea wetu walikatwa bila sababu za msingi, tukapambana kuanza kukata rufani, lakini wakati tunaendelea kufanya hivyo, hata wale wachache nao wameenguliwa kuanzia jana (juzi) na leo (jana), na mpaka tunavyozungumza sasa karibu nchi nzima, engua engua inaendelea.

"Hii ni hatari sana na hali hii ikiendelea kuwa hivi, tunasubiri tuone wanatuachia wagombea wangapi, halafu sisi kama chama tutajitathmini, tutaeleza kwa umma, ni nini ambacho kimetokea kwenye uchaguzi huu," alisema Mrema.

Mrema aliitaka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), kutoka hadharani na kuelezea umma kuhusu hali hiyo ya wagombea kuenguliwa.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa ACT-Wazalendo, Rahma Mwita, alisema mpaka jana, wagombea wao 51,423 nchi nzima walikuwa wameenguliwa na kuitaka ofisi hiyo inayosimamia uchaguzi huo, kuwarejesha walioenguliwa.

"Ni jambo la kustaajabisha, tunamtaka Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa kutoka hadharani na kuwataka Wasimamizi wa uchaguzi kuwarejesha wagombea wetu wote walioenguliwa maana sababu walizozitaja za kuwaengua, hazina mashiko. Uvumilivu wetu una kikomo," alisema Rahma.

Ofisa Sheria Mwandamizi wa TAMISEMI, Mihayo Kadeke, akizungumza kwenye moja ya radio, alisema kanuni za uchaguzi zinatoa nafasi kwa ambao hawajaridhika na maamuzi ya msimamizi msaidizi wa uchaguzi huo, kukata rufani, wanatakiwa watumie fursa hiyo kupata haki yao.

"Kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, baada ya uteuzi kufanyika na msimamizi msaidizi, Novemba 8, alibandika majina ya walioteuliwa na ambao hawakuteuliwa kwa kukosa sifa, lakini kanuni zinatoa nafasi kwa wale ambao hawajaridhika na uamuzi huo, kuweka pingamizi dhidi ya uamuzi aliokuwa ameufanya," alisema Kadeke.

"Na pingamizi hizo zilipaswa kuwasilishwa kwenye ofisi ya msimamizi kuanzia Novemba 8 na 9, halafu baada ya hapo, msimamizi msaidizi, alikuwa na siku mbili za kutoa maamuzi baada ya kupokea yale mapingamizi.

"Kwa mujibu wa kanuni, tunatambua kwamba kuna watu pamoja na kuweka pingamizi, wanaweza wasiridhike pia na yale maamuzi ya msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kwa hiyo, mtu kama hatoridhika, atakuwa na haki ya kwenda kukata rufani kwenye kamati za rufani kwenye kila wilaya.

"Kamati hizi zimeundwa kwa mujibu wa kanuni, kwa ajili ya kusikiliza hayo malalamiko au maamuzi yaliyofanywa na msimamizi msaidizi wa uchaguzi ambayo hayajawaridhisha kwa namna moja au nyingine, ikiwamo pia kuenguliwa katika hizo nafasi. Kwa hiyo wana muda wa kuwasilisha rufani zao kwa kamati ya rufani ambayo imeanza tarehe 10 na itafanya kazi mpaka tarehe 11, 12 na 13."

Ofisa huyo alisema kamati hizo ni huru na zina wajumbe ambao hawajashiriki kwa namna yoyote kwenye uteuzi wa wagombea.

"Kwa hiyo tunaamini kama mtu akitumia fursa hiyo ya kukata rufani kwenye hizo kamati, kama haki yake ilidhulumiwa au kama alikuwa na sababu za msingi, basi kamati itatenda haki ili mgombea huyo ambaye aliengulliwa au mwingine ambaye hajaridhika na uwapo wa wagombea fulani, uamuzi utendeke kwa haki.

"Kama wizara, hatujapata taarifa rasmi, kwa sababu uchaguzi unafanyika chini kwenye halmashauri na kipindi hiki chote ni cha uchaguzi, tunategemea ofisi ziwe wazi na wahusika wawepo ili watu wasikose haki zao, hivyo, kama kuna maeneo yana malalamiko, wana fursa ya kuwasilisha kwenye mamlaka husika ili haki itendeke," alisema Kadeke.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa (NEC) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla akizungumza na wanachama pamoja na viongozi wa chama hicho wilaya ya Mkuranga kwenye Uwanja wa CCM wilayani humo jana. **PICHA: CCM**

# CCM tumewekewa mapingamizi na tunaamini haki imetendeka - Makalla

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, amewaomba wanachama katika maeneo ambayo wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamewekewa mapingamizi, kuwa watulivu kwa kuwa chama hicho kinaamini haki itatendeka kwa vyama vyote.

Makalla aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi na wanachama wa CCM wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, akisisitiza CCM itaibuka na ushindi wa haki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliopangwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu.

"Niwaombe wana CCM, tupo katika hatua za mapingamizi. Sasa hivi kinachoendelea mitandaoni ni malalamiko ya vyama vya upinzani kuonesha kama vile pekee ndiyo waliowekewa mapingamizi.

"Wanafanya hadaa, upotoshaji wa takwimu feki na kujisahaulisha kwamba hata wagombea wa CCM wamewekewa mapingamizi.

"Juzi nilisema tunaamini TAMISEMI itatenda haki kwa vyama vyote kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki na atakayeshinda atangazwe kwa haki.

"Kwa hesabu zetu na wagombea tuliowaweka, tunaamini CCM tutashinda kwa haki. Kwa hiyo, rufani zinaendelea, baada ya uteuzi wa wagombea, CCM itatoa taarifa baadaye," alisema.

Makalla pia alikemea tabia hiyo ya baadhi ya vyama vya upinzani kufanya alichokiita "kupotosha umma" kwamba wagombea wa vyama hivyo pekee ndiyo wamewekewa mapingamizi wakati si kweli.

Alisema kuwa vyama vyote, ikiwamo CCM, ambavyo wagombea wake wamewekewa mapingamizi ya kuteuliwa, vinaendelea kukata rufani kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Niwaombe wanaCCM katika maeneo ambayo tumewekewa mapingamizi, tuwe watulivu, tukiamini haki itatendeka kwa vyama vyote," alisisitiza Makalla.

Mwenezi huyo pia alimpongeza Mbunge wa Mkuranga ambaye pia ni Waziri wa Mifugo, Abdallah Ulega kwa kutoa vitendea kazi, zikiwamo baiskeli kwa viongozi wa CCM katika wilaya hiyo.

Alisema vifaa hivyo vimetolewa katika muda mwafaka kusaidia ushindi wa CCM.

"Mkazitunze baiskeli, mkazifanyie kazi na utaratibu mzuri utawekwa, akiitaka mwenyekiti aitumie, akiitaka mwenezi aitumie, yote ni kwa ajili ya Chama Cha Mapinduzi," alisema Makalla.

Naye Ulega alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufungua wilaya hiyo katika sekta mbalimbali muhimu kwa maendeleo ya wananchi.

"Rais Samia ni tunu na kiongozi wetu imara, tunajivunia sana kwa wilaya ya Mkuranga ametufanyia mambo makubwa katika sekta ya elimu, afya, miundombinu, maji na umeme," alieleza Ulega.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kambi za upimaji afya zinasaidia wasiojiweza

**UTARATIBU** wa kuanzisha kambi maalumu zinazosaidia wananchi wasioweza kumudu gharama, kupima afya umesaidia kugundua magonjwa mengi na kutoa fursa ya kusaidiwa matibabu.

Utaratibu huu umesaidia wananchi wengi kugundua maradhi ambayo walikuwa hawajui kama wanayo na hatimaye kupatiwa tiba.

Kuna watu wanatembea na maradhi ambayo sio rahisi kuyagundua mpaka watakapokwenda kwa wataalam kupimwa.

Wakati Waziri wa Afya akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya bajeti ya wizara yake bungeni, alisema serikali inakusudia kuja na chombo muhimu kitakachokuwa kinadhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi.

Afya ni muhimu katika maisha ya binadamu hivyo ni lazima suala la gharama liangaliwe ili lisiwaumize wananchi hasa wasiokuwa na uwezo.

Kwa kuanzishwa chombo chenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi hususan wasio na bima ya afya, malalamiko yatapungua.

Utaratibu huu utasaidia kudhibiti utozaji gharama holela unaofanywa na baadhi ya madaktari katika hospitali za binafsi na zile za serikali ili kuwapa unafuu wananchi.

Vyombo kama hivi vimefanikiwa pia katika huduma za mafuta ya petroli ambapo inafahamika kila mtu anapokwenda kwenye kituo cha mafuta kujaza kwenye gari yake anakuta bei elekezi.

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa wanapokwenda kutibiwa kukuta wakitozwa gharama kubwa kumuona daktari kabla ya kupata matibabu, hali inayowafanya wasiokuwa na bima za afya kushindwa kulipia na kuamua kwenda kujaribu tiba zingine mbadala.

Kwa mujibu wa wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Fedha, kwenye vitita vya NHIF, madaktari bingwa katika ngazi ya rufani mkoa, ada imeongezeka kutoka Sh. 15,000 hadi 25,000 ambayo ni sawa na kumuona daktari aliyepo ngazi ya kanda na taifa.

Kiwango hiki cha kumuona daktari kinatoa hamasa kwa madaktari hao kufanyakazi katika mazingira yoyote watakayopangiwa, ikiwamo pembezoni.

Aidha, ada ya usajili na kumuona daktari kwa wanufaika wa NHIF kwa ngazi ya wilaya imeongezeka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 7,000 kwa ngazi ya zahanati ada imeongezeka kutoka Sh. 1,000 mpaka Sh. 3,000.

Aidha, kitita hicho kitaboresha upatikanaji wa huduma bora za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wanachama.

Aidha, kitita hicho kimezingatia maendeleo ya teknolojia ya tiba, hali halisi ya bei katika soko na uwezo wa mfuko kugharamia huduma hizo huku ukiendelea kuwa endelevu kwa kuzingatia ushauri wa taifa, mapendekezo ya tathmini ya uhai na uendelevu.

Wizara ya Afya pia imetaja vipaumbele na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.


Katika bajeti hiyo wizara imetenga Sh. bilioni 117.61 kuimarisha huduma ya kinga dhidi ya magonjwa ikiwamo kuimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa kuwafikia watoto 3,117,564 wenye umri chini ya miaka miwili, wasichana 871,429 wenye umri wa miaka tisa na wajawazito 3,298.437.

Kwa mujibu wa waziri, Sh. bilioni 17.18 zimetengwa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, ikiwamo kujenga, kukakarabati na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa waliozaliwa na uzito upungufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Dua njema kidato cha nne 2024

**WANAFUNZI** wa kidato cha nne wameanza mitihani ya taifa kukamilisha safari ya kuhitimu daraja hilo la taaluma.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Said Mohamed wakati akitangaza kuanza kwa mtihani huo Jumatatu wiki hii ukitarajiwa kuendelea hadi mwisho wa mwezi huu ifikapo Novemba 29.

Anasema idadi ya wa watahiniwa mwaka huu ni 557, 731, ambao ni wa shule na wengine wa vituo vya kujitegemea maarufu QT.

Wakati wanafunzi wakiwa katika mtihani huo, ni vyema kuendelea kuwakumbusha kujitenga na kila aina ya udanganyifu, badala yake waufanye kwa kuzingatia utararibu unaokubalika, si vinginevyo.

Ninakumbushia hilo, kwa sababu ni karibu kila mwaka baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakifutiwa matokeo ya mtihani kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni kufanya udanganyifu.

Hivyo, ingekuwa ni vyema kama mtindo huo wa udanganyifu utafikia kikomo, ili wanafunzi wafanye mtihani na kutegemea akili zao kutokana na kile ambacho wamefundishwa kwa muda wa miaka minne.

Mfano, katika matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana, wanafunzi 102 walifutiwa matokeo yao baada ya kubainika wamefanya udanganyifu, wakiwamo wengine walioandika matusi kwenye karatasi za majibu.

Sidhani kwamba, kwa miaka minne kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, wanafunzi wanafundishwa kufanya udanganyifu au kuandika matusi kwenye karatasi za majibu. Hiyo ni tabia mbaya inayotakiwa kuachwa.

Wanafunzi wa kidato cha nne wanaandaliwa kusonga mbele kielimu ili baadaye waje walisaidie taifa lao katika nafasi mbalimbali kulingana na kile ambacho watakuwa wamekisomea.

Ufaulu wa mtihani wenye udanganyifu hauwezi kusaidia taifa kupata wataalam bora wa wa fani mbalimbali watakaolisaidia kwa miaka ya baadaye. Hivyo, mtindo huo ungekemewa na kila mdau wa elimu.

Ingekuwa ni vyema walioanza mtihani wa taifa wa kidato cha nne mwaka huu waonyeshe mfano bora wa kutojihusisha na kila ya aina ya udanganyifu ili isiendelee kujengeka vichwani mwa wanafunzi kuwa udanganyifu ni sehemu muhimu katika mtihani huo.

Katika mazingira hayo, wanafunzi wengine wasio na tabia hiyo, wanaweza kushawishika na kujikuta wameingia kwenye mtego wa kutegemea udanganyifu badala ya akili zao.

Vilevile, ikumbukwe kwamba, hadi mwanafunzi anafanya udanganyifu katika mtihani, maana yake kuna baadhi ya walimu na wadau wengine wa elimu wamehusika kwa namna moja au nyingine.

Hivyo, ungefanyika ufuatiliaji wa kina ili kubaini mianya yote inayosababisha kuendelea kwa vitendo hivyo na kuwachukulia hatua kali wahusika ili wasiendelee kuvuruga utaratibu wa ufanyaji mitihani.

Ikiwezekana, kila shule iwe na kitengo cha udhibiti ubora kinachosimamia mfumo mzima wa ufundishaji kutoka utungaji wa mitihani, usahihishaji hadi matokeo.

Lakini pia si vibaya kama kutakuwa na mfumo wa kumtambua mtahiniwa kwa alama za vidole kabla hajaingia katika chumba cha mtihani, ili kuwadhibiti wale wanaotoa fedha kwa lengo la kufanyiwa mitihani waweze kufaulu kwa kutumia akili za wengine.

Hata hivyo, ninadhani ipo haja sasa wadau wa elimu kuangalia uwezekano mwingine ambao wanaona unafaa kupima uelewa wa mwanafunzi nje ya mtihaani ambao sasa unaingiliwa na danganyifu.

Mfumo wetu wa elimu kupimwa uelewa wa mwanafunzi kumejikitika katika mitihani kuanzia darasa la kwanza, lakini si vibaya kama wataalam wetu watakuja na njia mbadala wa mitihani.

Pamoja na hayo, niwatakie kila la heri wanafunzi wa kidato cha nne walioanza mtihani wao wa taifa kwa mwaka 2024, wajiepusha na udanganyifu, watumie akili ili wafaulu kihalali.

# Watumishi watimuliwa kwa utoro kazini

**Na Judith Julius,** NGARA

KAMATI ya Maadili ya Baraza la Madiwani wilayani Ngara imeridhia kufukuzwa kazi watumishi watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa kosa la utoro kazini.

Watumishi waliofukuzwa kazi ni pamoja na Ofisa Mtendaji wa Kata, Venance John, Ofisa Lishe Daraja la Pili Audivance Shirima na Ofisa Tabibu Daraja la Pili Elizabeth Minja.

Akisoma taarifa ya uamuzi huo mbele ya Mwenyekiti wa Halmashauri, Wilbard Bambara, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mkiza Byamungu alisema wamefikia uamuzi huo kutokana na wafanyakazi hao kukiuka maadili, kanuni na taratibu za utumishi.

Byamungu alisema sababu za kufukuzwa kazi ni utoro wa muda mrefu bila taarifa yoyote ambako Venance hakwenda kwenye kituo chake zaidi ya siku tano, Shirima hakuwapo kazini zaidi ya miezi minane na Elizabeth hakuwapo katika kituo cha kazi kwa zaidi ya miezi mitatu.

"Ni dhahiri kuwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za kazi kuwapo kwa watumishi hao nje ya vituo vyao vya kazi ni kosa la kukusudia na utoro kazini," alisema Byamungu.

Alisema kamati imefikia hatua hiyo kwa mujibu wa kanuni za kudumu za utumishi wa umma ambazo zinatoa adhabu ya kufukuzwa kwa mtumishi aliyekaa nje ya majukumu yake zaidi ya siku tano.

Alisema kwa mujibu wa kanuni hizo, wafanyakazi hao wamebainika kutenda kosa hilo na hivyo wanastahili kufukuzwa kazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Bambara, aliwataka watumishi wafanye kazi kwa kufuata taratibu, sheria na kanuni za utumishi na wasifanye kazi kwa mazoea.

Bambara alisema baraza limekubaliana kufukuza watumishi hao watatu waliokimbia maeneo ya majukumu yao, lakini halijui sababu zilizowafanya wakimbie kwa kuwa hakuna aliyempa taarifa mwajiri wake.

Vilevile, aliwasihi madiwani kuwa karibu na watumishi ili kuwasikiliza na kuwashauri, hata kuondoa hali ya kufukuzana kazi kutokana na utoro.

Alimshauri Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Salmon Kimilike, kuwatendea haki watumishi pale inapotakiwa kwa kuwa akiwa msikivu kwao, atawasaidia kupenda mazingira wanayofanyia kazi na kuongeza bidii.

"Wapo watumishi wengi wanoidai halmashauri, hivyo endeleeni kuwalipa ili waweze kukidhi mahitaji yao," alielekeza.

**Byamungu alisema sababu za kufukuzwa kazi ni utoro wa muda mrefu bila taarifa yoyote ambako Venance hakwenda kwenye kituo chake zaidi ya siku tano, Shirima hakuwapo kazini zaidi ya miezi minane na Elizabeth hakuwapo katika kituo cha kazi kwa zaidi ya miezi mitatu.**




Mkurugenzi wa Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC), David Kafulila akitoa mafunzo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) hawapo pichani, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya kituo hicho ambacho kimeshaandaa miradi 84. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yaokoa mamilioni ya shilingi ugawaji viuatilifu wakulima wa korosho

**Na Baraka Jamali,** MTWARA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mtwara imeokoa zaidi ya Sh. milioni 31.4 zilizokuwa zimeelekezwa kwa matumizi yasiyo halali katika msimu wa kilimo cha korosho 2024/25.

Ni hatua iliyolenga kuhakikisha rasilimali zinawafikia walengwa sahihi bila kuingiliwa na vitendo vya rushwa au ubadhirifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, Jumbe Makoba, alisema kuwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2024, kupitia kampeni maalumu ya TAKUKURU Rafiki, walifanikiwa kutatua changamoto za wakulima wa korosho katika kijiji cha Chinyanyira, kata ya Sengenya, wilaya ya Nanyumbu.

Kampeni hiyo iliibua kadhia ya baadhi ya wakulima kupunjwa viuatilifu vya aina ya sulphur, huku wengine ambao hawana mashamba ya mikorosho wakigawiwa bidhaa hiyo kinyume na utaratibu.

Makoba alisema, "Katika uchunguzi wetu, tulibaini kuwa mifuko 604 ya viuatilifu vyenye thamani ya Sh. milioni 31.408 ilikuwa imepangwa kugawiwa kwa wakulima wasio na miti ya mikorosho, hali iliyosababisha wale wenye mashamba halali kukosa bidhaa hizo muhimu."

Alisema kuwa kupitia jitihada za TAKUKURU na kwa kushirikiana na wadau wengine, mifuko hiyo ilirejeshwa katika mfumo rasmi na kugawiwa kwa wakulima waliokuwa wamenyimwa viuatilifu hivyo.

Kwa mujibu wa TAKUKURU, operesheni hiyo ni moja ya hatua muhimu za kufanikisha malengo ya kampeni ya TAKUKURU Rafiki inayolenga kuwa karibu zaidi na jamii kwa kusikiliza na kutatua changamoto zao.

Makoba aliwahimiza wakulima na wananchi wote kushiriki kwa uwazi katika utoaji taarifa kuhusu rushwa ili kudhibiti vitendo hivyo vinavyoathiri maendeleo ya jamii.

Pamoja na hatua hiyo, TAKUKURU imeendelea kutoa elimu ya udhibiti wa rushwa kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika tarehe 27 ya mwezi huu.

Makoba alieleza kuwa kampeni ya uhamasishaji jamii inakwenda sambamba na kutoa elimu ya namna ya kujiepusha na vitendo vya rushwa katika uchaguzi huo na kuwaonya wale wote wenye nia ya kuharibu mchakato huo kwa kutoa au kupokea rushwa.

"Tunatoa wito kwa wananchi wote kujiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi huu na pia kutoa taarifa katika ofisi yoyote ya TAKUKURU iwapo watashuhudia vitendo vyovyote vya rushwa.

"Vilevile, tunahimiza watoa huduma na wale wanaosimamia miradi ya maendeleo kuwa waadilifu na kuzingatia kanuni za uadilifu ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa manufaa ya umma," alisema Makoba.

Kwa mujibu wa TAKUKURU, takwimu zinaonesha kuwa matukio ya rushwa katika sekta ya kilimo yanazuia ustawi wa wakulima na kusababisha hasara kubwa kwa taifa.

Kutokana na changamoto hizo, Makoba alisema TAKUKURU inaendeleza juhudi za kupambana na ufisadi kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufuatilia, kutoa elimu na kuchukua hatua kali kwa wote wanaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Makoba alisisitiza kuwa TAKUKURU imejipanga kikamilifu kusimamia na kudhibiti ubadhirifu wa rasilimali za umma, hususani katika kipindi hiki ambacho taifa linaelekea kwenye uchaguzi.

Alisema kuwa ni wajibu wa kila raia kushiriki katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa njia ya haki, uwazi na bila kuingiliwa na vitendo vya rushwa.

Kampeni ya TAKUKURU Rafiki ni moja ya mikakati ya taasisi hiyo ya kuwa karibu na jamii kwa kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wananchi.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# ATCL yapunguza gharama za uendeshaji

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imepongeza ubunifu wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) wa kupunguza gharama za uendeshaji kupitia uboreshaji wa karakana zake.

Karakana za Kampuni hiyo ziko katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Selemani Kakoso, alitoa pongezi hizo baada ya kutembelea karakana ya matengenezo ya ndege na eneo itakapojengwa mpya.

Alisema wanaridhishwa na hatua zinazochukuliwa na ATCL katika kudhibiti gharama za uendeshaji.

Aidha, alisema kukamilika kwa taratibu za umiliki wa ndege kutoka Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania (TGFA) kwenda Kampuni ya Ndege Tanzania, kutaongeza ufanisi zaidi ikiwamo kuondokana na deni kubwa linaloonekana kwenye hesabu za ATCL.

"Kwa sababu taratibu za kuhamisha umiliki zimeshaanza, Kamati tunaendelea kushauri Serikali kukamilisha zoezi hilo ili kupunguza deni la ATCL kwenye vitabu. Kwa kufanya hivyo, mapato na matumizi halisi ya ATCL yataonekana," alisema Kakoso.

Aliipongeza serikali kwa kuendelea kuimarisha ATCL kwa kuongeza ndege ili kutanua mtandao wa safari.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Oran Njeza, alisema kamati imeona miradi mikubwa ya ATCL ikiwamo ujenzi wa karakana na mikakati wa kuboresha muundo wake wa utendaji ili kuendana na matakwa ya biashara.

Naibu Waziri wa Wizara ya Uchukuzi, David Kihenzile, alizishukuru kamati zote mbili na kuahidi kufanyia kazi maoni na mapendekezo yote kwa kushirikiana na kamati katika kutatua changamoto zinazoikabili ATCL.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL Mhandisi Ladislaus Matindi, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuiwezesha ATCL kuboresha karakana na kuruhusiwa kufanya matengenezo makubwa ya ndege kwa kiwango cha C - Check.

Alisema awali ATCL ilikuwa haina uwezo hata wa kubadilisha tairi linapopata hitilafu na kuwalazimu kusafirisha Nairobi kwa ajili ya kuzibwa pancha.

Matindi alisema kitendo cha watengeneza ndege kutoa kibali cha matengenezo makubwa kufanyika nchini ni uthibitisho wa kutimiza vigezo na utaalamu wa kufanya matengenezo hayo.

Kuhusu ATCL kutanua mtandao wake wa safari, alisema kwa sasa imeshaanza mauzo ya tiketi za Johannesburg na safari ya kwanza itakuwa Novemba 30, 2024.



Mgombea ujumbe wa serikali ya mtaa wa Mzinga, kata ya Mzinga jijini Dar es Salaam, kwa tiketi ya CCM, Mwanahamisi Kassim (kushoto) akipokea fedha kutoka kwa mwenyekiti wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Fatma Twalib juzi, kwa ajili ya kampeni. Fedha hizo zimetokana na mkakati wa kituo hicho wa kuhamasisha wanawake wajasiriamali kuchangishana Sh.200 kila siku kwa miezi miwili ili kuwawezesha wenzao wenye nia ya kuwania uongozi, ambapo sasa wapo 12 wanaowania uongozi kutoka vyama vyote wamepewa Sh. 100,000 kila mmoja za kufanyia kampeni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kishapu wadai kupokea mbegu 'feki', maofisa ugani walalama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAOFISA Ugani wa Halmashauri Wilaya ya Ushetu mkoani Shinyanga wamedai mbegu za pamba zilizoanza kusambazwa wilayani humo kwa ajili ya msimu wa kilimo 2024/25, hazina ubora na kuiomba serikali kuzichunguza kabla hazijaanza kutumiwa na wakulima.

Maofisa hao akiwamo Dismas Minja wa Kata ya Mwanga, walitoa malalamiko hayo juzi katika kikao cha pamoja baina yao na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, Watendaji Kata pamoja Balozi wa pamba nchini, Aggrey Mwanri.

Minja alisema mbegu za pamba walizoletewa kwa ajili ya kuzisambaza kwa wakulima, zimeonekana kutokuwa na ubora na hazifai kwa kilimo katika msimu unaoanza na kuomba mkuu huyo wa mkoa kuzichunguza na wakulima wapatiwe mbegu nyingine zinazostahili.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, alikiri kupokea malalamiko kuhusu ubora wa mbegu za pamba zilizosambazwa kwa wananchi katika msimu wa 2023/24 na kuwa sio nzuri, na tayari amerudishiwa baadhi ya mifuko kutoka kwa wakulima ambao wamekataa kuzitumia.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Anamringi Macha, alitoa siku saba kwa bodi ya pamba, kufanya ukaguzi wa ubora wa mbegu hizo na kisha kumpatia taarifa.

"Kazi niliyotumwa na Rais Samia Suluhu Hassan ni kurudisha heshima ya pamba na kazi ambayo anaifanya Balozi wa pamba, Aggrey Mwanri, bila ya kuwapo kwa ubora wa mbegu za pamba itakuwa bure hivyo TCB mnapaswa kufanya ukaguzi wa mbegu zote zinazosambazwa wilayani hapa ili wakulima walime kwa ubora," alisema Macha.

Aliwataka kujihakikisha kama mbegu hizo zinafaa, kama hazifai kuleta mbegu nyingine zenye ubora, ili kazi hiyo ambayo wametumwa na Rais ifanyike kwa ufanisi.

Mkaguzi wa pamba wilayani Kishapu kutoka Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Thomas Tiluhongerwa, akiangalia sehemu ya mbegu zinazoelezwa kuwa ni mbovu, alikiri kuwa sio nzuri kwa matumizi na kuzifanyia uchunguzi mbegu zote wilayani hapo na kumhakikishia kumpa taarifa ndani ya siku saba.

## Programu ufanisi wa nishati kuleta mabadiliko ya kisekta

**Na Maulid Mmbaga**

PROGRAMU ya ufanisi wa nishati italeta mabadiliko ya kisekta nchini katika kuimarisha mifumo ya kisheria, udhibiti, kitaasisi, kiutawala, kutoa usaidizi kwa watumiaji wakubwa, wa jumla, ukuzaji wa uwezo na ujuzi kwa vijana.

Prograramu hiyo pia inalenga kuongeza uelewa wa umma na mwonekano wa manufaa ya kiuchumi, kifedha, kimazingira na kijamii ya ufanisi wa nishati na nishati mbadala.

Hayo yalielezwa na Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Wilson Nyamanga, ambaye pia ni Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala, katika hafla ya utoaji wa vyeti vya ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 25 ngazi ya Shahada za Uzamili katika Uhandisi wa Nishati Endelevu, iliyofanyika juzi mkoani Dar es Salaam.

"Mpango wa utekelezaji wa ufanisi wa nishati, ambao tunatekeleza, umeundwa ili kuziba pengo la kijinsia katika sekta ya nishati, kwa kuweka kipaumbele katika ukuzaji wa ujuzi na sifa za kitaaluma katika usimamizi na ukaguzi wa nishati.

"Kuwawezesha wataalamu zaidi, hasa wanawake, kuwa na ujuzi katika maeneo haya kwa kutambua kwamba wafanyakazi wenye ujuzi ni muhimu katika kuendeleza malengo ya ufanisi wa nishati ya Tanzania na kukuza maendeleo endelevu katika sekta nzima," alisema Nyamanga.

Aliongeza kuwa mpango huo kwa awamu ya kwanza ulichukua wanafunzi wanawake 10 na hadi sasa wamefikia 35 hatua itakayosaidia kuleta mafanikio makubwa kuelekea maono yao ya nguvu kazi ya nishati jumuishi.

Aidha, alisema wapokeaji wa ufadhili huo wanawakilisha mustakabali wa sekta ya nishati, na mafanikio yao yatachukua jukumu muhimu katika kuunda mazingira endelevu na jumuishi ya nishati katika taifa.

Alisema hivi karibuni watazindua Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Jadidifu na Mkakati wa Kitaifa wa Ufanisi wa Nishati ambao ni muhimu kwa mustakabali wa nishati ya Tanzania na mafanikio yake yatategemea wafanyakazi wenye ujuzi wa hali ya juu.

Kaimu Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Muyeye Chambwera, alisema kukuza usawa wa kijinsia katika sekta ya nishati si tu suala la usawa ni mkakati madhubuti wa kufikia Malengo Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa (SDG 5) kuhusu usawa wa kijinsia.

"Pia utasaidia kufikia malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 7) kuhusu nishati nafuu na safi. Mitazamo ni utaalamu wa kipekee wa wanawake ni muhimu kwa ajili ya kuendesha uvumbuzi na kukabiliana na changamoto tata tunapojitahidi kukidhi mahitaji ya nishati ya Tanzania kwa uendelevu," alisema Chambwera.

Programu hiyo inatekelezwa katika Taasisi ya Teknolojioa Dar es Salaam (DIT) chini ya ufadhili wa UNDP Tanzania, Umoja wa Ulaya (EU) na Ubalozi wa Ireland.



# Kesi ya m/biashara, wenzake yapigwa kalenda

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, imesogeza mbele kesi ya uhujumu uchumi, inayomkabili mwekezaji na mfanyabiashara, Saleh Alamry (54) na mwenzake, huku ikiagiza kukamilishwa haraka upelelezi wake ili kutenda haki kwa washtakiwa.

Hakimu Mfawidhi wa mahakama hiyo, Erasto Philly, alisema licha ya upande wa mashtaka kuieleza mahakama kwamba, upelelezi utakamilika ndani ya wiki moja kuanzia sasa, hataki mahakama itumike kama ngazi ya kuchelewesha haki.

Baada ya shauri hilo kutajwa, wakili wa serikali, Ahmed Mbagwa, alidai kuwa upelelezi bado haujakamilika, huku akiahidi kukamilisha ndani ya wiki moja.

Mwekezaji Alamry, yuko mahabusu ya Gereza Kuu la Arusha la Kisongo, kwa zaidi ya siku 80 sasa, tangu alipokamatwa Agosti 22 mwaka huu akikabiliwa na makosa 27, yakiwemo ya uhujumu uchumi, utakatishaji wa fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani milioni 26.

Jopo la mawakili wa utetezi linaongozwa na wakili Faisal Rukaka na wenzake Moses Mahuna na Denis Mworia.

"Tumesikia upande wa Jamhuri wakidai upelelezi bado, ila wanatarajia wiki ijayo wawe wamekamilisha. Katika muktadha huo, tunaomba Ofisi ya DPP (Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka), itoe consent kwa mahakama hii (hati au ruhusa au mamlaka) ili isikilize kesi hii na kutoa baadhi ya amri.

"Tunaomba suala hili la upelelezi lifanyike kwa haraka, kwa sababu kosa la mteja wetu halina dhamana na anakosa kufanya shughuli zake za kila siku."

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi, imehairishwa hadi Novemba 21 mwaka huu, itakapotajwa tena mahakamani humo.

**Jopo la mawakili wa utetezi linaongozwa na wakili Faisal Rukaka na wenzake Moses Mahuna na Denis Mworia.**

# Kamati yatoa maagizo upandaji miti ya matunda, vivuli Hanang'

**Na Jaliwason Jasson,**
HANAN'G

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, imeelekeza serikali ya Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara, kuwezesha upandaji wa miti ya matunda na vivuli katika makazi mapya 109 ya waathirika wa maporomoko ya tope na mawe ya Hanang.'

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jackson Kiswaga, alitoa maelekezo hayo jana baada ya kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi za waathirika hao.

"Kamati yangu imeridhishwa na ujenzi wa nyumba hizi. Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA), wamefanya kazi kubwa ya kuunganisha maji kwenye makazi haya.

"Tunataka kabla ya Rais, Samia Suluhu Hassan kuja kuzindua makazi haya, kuwe kumepandwa miti ya kutosha ya matunda na vivuli. Rais ni mwana mazingira halisi, ni vizuri eneo la makazi ya waathirika wa maporomoko ya mawe na tope ipandwe miti, itasaidia sana pia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi."

Mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Nyasa, Stella Manyanya, alisema ni vizuri uangaliwe mfumo wa maji taka, kwa kuwa watu wanaokuja kuishi hapo wamezoea kuishi vijijini na kila mtu ana eneo lake.

Hivyo, alishauri ni vyema viwekwe vifaa vya kutupa taka, ili kuepusha magonjwa ya mlipuko.

Kwa upande wake, Mbunge wa Hanang,' Samweli Hhayuma, aliishukuru serikali kwa kuwajengea nyumba wananchi wake.

Akitoa taarifa ya namna maji yalivyoingizwa kwenye nyumba hizo, Meneja wa RUWASA-Manyara, James Kionaumela, alisema nyumba zilizounganishiwa huduma ya maji ni 109.

Alisema serikali imejenga nyumba 73, Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross) imejenga nyumba 35, na nyumba moja ilijengwa na Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT).

Kwa mujibu wa Kionaumela, fedha iliyotolewa kuunganisha maji ni Sh. milioni 157.

Alisema: "Hiyo Sh.milioni 157 ni katika shilingi bilioni 5.2, ambayo imetumika kupeleka maji vijijini, tukijumuisha na ya mjini inakuwa shilingi bilioni tisa. Yote imetumika sekta ya maji tu kurejesha miundombinu".



Wanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Muheza Muslim iliyopo wilayani Muheza mkoani Tanga jana wakiwa mapumziko kwenye mtihani wa Taifa wa kidato cha nne ambao jumla ya watahiniwa 2288 wanafanya mtihani wa Taifa wa kidato cha nne wilayani Muheza ambao wavulana 1075,Wasichana 1213 na watahiniwa wenye mahitaji maalum 27, wametoka katika shule za Sekondari 29 wilaya ya Muheza ambazo za Serikali 24 na binafsi tano. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yapunguza miradi ya maji kichefuchefu

**Na Jaliwason Jasson,**
HANANG'

NAIBU Waziri wa Maji, Mathew Kundo, amesema kasi ya uboreshaji miradi ya maji nchini ambayo ilikuwa kichefuchefu imepungua kutoka 177 hadi 164.

Akizungumza jana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira katika Mji wa Katesh, mkoani Manyara, Naibu Waziri huyo, alisema miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na ya Mkoa wa Manyara.

Kamati hiyo ilikwenda kukagua miradi ya maji iliyokuwa imeharibiwa vibaya na maporomoko ya mawe na tope ya Hanang, ambayo sasa imerejeshwa.

Jumla ya kaya 207 zilizokuwa na wakazi 322 zilipoteza makazi katika Mji wa Katesh, vijiji vya Jorodom, Ganana, Katesh, Dumbeta, Gendabi, Sarijandu, Arukushay na Sebasi, baada ya maporomoko ya mawe, magogo na matope yaliyosababishwa na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia Desemba 3 mwaka huu.

Kundo alisema, "Shilingi bilioni 114 zimeshaletwa Mkoa wa Manyara, kwa ajili ya miradi ya maji na miradi ya kimkakati inaendelea kutekelezwa.

Hata hivyo, baada ya Waziri wa Maji, kupeleka ombi la kuchimba visima 900, kwa Rais (Samia Suluhu Hassan) aliridhia, ili wakati juhudi zinafanyika wananchi wawe wanapata maji, hivyo mpango huo umesaidia kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji."


Alisema maporomoko ya mawe na tope, yaliathiri miradi miwili ya maji, ambapo serikali ilitoa Sh. bilioni tisa kwa ajili kurejesha miundombinu hiyo ya maji.

Kutokana na maelezo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Jackson Kiswaga, alisema kamati yake imeridhika na kazi iliyofanywa na wataalamu wa maji ya kurejesha miundombinu ya maji iliyoharibiwa na maporomoko ya mawe na tope.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akizungumza na wabunge hao alisema kwa sasa mkoa huo, kwa mjini upatikanaji wa maji ni asilimia 84 na vijijini ni asilimia 71, na wastani kwa ujumla ni asilimia 75.5.

Mbunge wa Vijana Taifa, Asia Halamga, alisema ilikuwa vigumu kuamini kama miundombinu ya maji iliyoharibiwa na maporomoko hayo ya Hanang' ingerejea haraka.

Kwa upande wake, Mbunge wa Hanang,' Samweli Hhayuma, alisema kazi iliyofanyika ni kubwa na sasa wananchi wa Mji wa Katesh, wanaoga maji saa 24.





# Wataja tiba udumavu, utapiamlo kwa watoto

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WADAU wa makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto wamesema kuzidi kwa hali ya udumavu wa akili pamoja na utapiamlo kwa watoto nchini kunahitaji ushirikishwaji na elimu ya mara kwa mara kwa wazazi.

Wamesema lengo ni kutambua namna ya kuchangamsha watoto pamoja na vyakula gani na muda gani wapatiwe kuimarisha lishe zao.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Shirika la TECEC, Joel Elphas wakati wa semina kwa wazazi jijini Mwanza iliyofanyika katika kituo cha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto cha shirika hilo.

"Katika kupambana na hali hii ya udumavu wa akili ni lazima mzazi awe sehemu ya kumuandaa mtoto kuanzia miaka sifuri mpaka nane akimfanyisha vitu vya uchangamshi, kumtengenezea zana mbalimbai za michezo zitakazomsaidia kumudu K tatu (kusoma, kuandika na kuhesabu) kabla hajaanza masomo," alisema Joel.

Kuhusu utapiamlo, Joel alisema siyo kwamba wazazi hawana vyakula vyenye lishe kwa ajili ya watoto wao bali hali ya mazoea na kutokufuata mlo kamili.

"Wazazi wanatakiwa kutambua namna ya kuandaa vyakula vinavyopatikana katika mazingira yao ili kutengeneza lishe bora kwa watoto wao na hii ndiyo elimu ya msingi tunayoitoa katika kituo chetu pamoja na kwenye mikutano mbalimbali ya lishe. Vilevile tunacho kituo cha kutengeneza unga wenye virutubishi kwa ajili ya watoto," alisema Joel.

Ofisa Maendeleo Mkoa wa Mwanza, Janeth Shishila alisema licha ya mapambano yanayofanywa na serikali kupitia wizara mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu kukabiliana na tatizo hilo bado ipo haja ya mashirika yasiyo ya kiserikali kusaidia katika kutokomeza janga hilo kwa watoto.

Alisema: "Shirika hili limekuwa mfano kwa kujenga kituo kwa ajili ya malezi na makuzi ya mtoto kikitoa malezi kwa watoto, elimu kwa wazazi na kujitolea ili kuhakikisha watoto wanakuwa na lishe bora na utimamu wa akili wote tuige mifano hii muhimu kwani serikali haiwezi kufanya kila kitu".



Balozi wa Pamba nchini Aggrey Mwanri akitoa mafunzo ya upuliziaji bora wa dawa ya kuua wadudu shambani katika kilimo cha zao la Pamba, kwa Maofisa Ugani wa Halmashauri ya wilaya ya Kishapu juzi ili elimu hiyo wakaitoe kwa wakulima. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Shule ya Sokoine yakumbwa uhaba walimu

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

UONGOZI wa Shule ya Msingi Sokoine iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, umeiomba serikali kuwaongeza walimu katika eneo hilo, ili kuhakikisha wanafunzi hao wanapata elimu bora.

Kwa mujibu wa mwalimu wa kitengo cha elimu maalum shuleni hapo, Pendo Labani, shule ina mwalimu mmoja ambaye anafundisha wanafunzi 30, hivyo kushindwa kuwafikia wanafunzi wote kwa wakati mmoja.

Tamko la Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 Kifungu cha 3(8) kinaitaka serikali kwa kushirikiana na wadau kuweka mazingira yatakayohakikisha watoto wenye ulemavu wanapata elimu jumuishi kwa kuzingatia mahitaji yao maalum.

Alisema upatikanaji wa viti hivyo umeondoa upungufu wa viti 25 uliokuwepo na kwamba vitasaidia kuleta hali ya utulivu katika kujifunza tofauti na ilivyokuwa awali.

"Tuliwaandikia wadau mbalimbali kuomba viti 25 ambavyo ndio ulikuwa upungufu, sasa tumeletewa viti 40 ambavyo vimevuka lengo, tunaushukuru uongozi kwa kujali ustawi wa watoto wenye mahitaji maalum," alisema Labani.

Meneja Biashara Kanda ya Magharibi, Anselm Mwenda alisema msaada huo ni utaratibu wao waliojiwekea wa kurudisha asilimia moja kwa jamii katika sekta ya elimu na afya hasa katika maeneo yenye mahitaji.

"Shule ya Msingi Sokoine haikuwa kwenye ratiba ya kupata mahitaji kwa wakati huu, lakini baada ya kupokea barua kutoka shuleni hapa na kuona wahitaji ni watoto wenye mahitaji maalum tulihairisha msaada uliokuwa umepangwa kupelekwa katika maeneo mengine ya nchi na kuuelekeza shuleni hapa," alisema Mwenda.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Rashidi Chuachua alisema bado kuna uhitaji mkubwa katika sekta ya elimu na kwamba serikali haiwezi kumaliza uhitaji huo bila msaada kutoka kwa wadau, hivyo kuwaomba waendelee kufanya katika maeneo mengi zaidi.

Vilevile Chuachua aliielekeza ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kigoma, kuweka utaratibu wa kuongeza walimu maalum kulingana na mahitaji ya watoto katika shule hiyo.

# Serikali yaingilia maandalizi kilimo cha pamba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imeanza kuingilia maandalizi ya mashamba ya pamba ili kuhakikisha wakulima wanalima kwa kufuata masharti.

Pia, imeahidi kuwachukulia hatua wakulima ambao bado hawajang'oa magugu shambani.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema hayo juzi kwenye kikao cha maofisa ugani na watendaji wa kata zote wilayani Kishapu, alipoambatana na balozi wa pamba nchini Aggrey Mwanri.

Alisema suala la kung'oa magugu shambani ni lazima kisheria kwani yanazalisha wadudu na ni hatari kwa shamba la mtu mwingine kushambuliwa na wadudu hao, ambaye tayari ameshasafisha shamba lake kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo cha pamba 2024/25.

"Natoa siku mbili tu za mwisho wakulima wote wa pamba wawe wameshang'oa magugu shambani, baada ya hapo ni kuwakamata na kuwachukulia hatua kali za kisheria kwani kung'oa maotea ni lazima siyo ombi maofisa ugani wilaya na kata simamieni hilo," alisema Macha.

Aidha, aliwataka maofisa hao ugani wakafanye kazi ya kusaidia wakulima wa pamba, kuwapatia elimu ya kilimo chenye tija, kwamba kipimo cha utendaji wao kazi katika msimu wa mwaka huu ni wakulima kuvuna kilo 800 kwa hekali moja kutoka wastani wa kilo 200.

Alisema kwa upande wa serikali, tayari wameshajipanga kurejesha heshima ya zao hilo, ambapo maofisa ugani walishapewa pikipiki, vishikwambi, vifaa vya kupimia udongo, sare, kuleta mbegu za pamba zenye ubora, pamoja na matrekta 24 ambayo yatapunguza gharama za kilimo kwa wakulima.

Naye, balozi wa pamba nchini, Aggrey Mwanri, alisema Septemba 15, mwaka jana ulikuwa mwisho wa kung'oa magugu shambani.

Alisema Novemba 15, mwaka jana itakuwa siku ya kuanza kupanda pamba lakini wakulima wengi wilayani Kishapu bado hawajang'oa magugu.

Hivyo, aliwataka pia wakulima wa pamba kutoichanganya na mazao mengine wakati wa kulima pamoja na kufuata kanuni bora za unyunyuziaji wadudu na uvunaji, huku akisisitiza kutoichafua pamba hiyo kwa kuweka mchanga, mawe na mafuta ya kenge.



Ukurasa 12

**Chumvi ni bora lakini ni hatari zaidi zama hizi**



Ukurasa 13


Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere kinavyolenga kuwa gwiji KITEHAMA

Nipashe

TESA

Jumanne Novemba 12, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Ni zamu ya kukipachika ubongoni usahaulifu huenda ukawa historia**

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

ZANZIBAR YAPAA KIUTALII

# Chanzo ubunifu, video za wapiga makachu zatikisa duniani kote

UBUNIFU unabadilisha namna ya kutangaza vivutio vya watalii Zanzibar. Ni kazi ya vijana wapigambizi wanaotumia mbinu na madaha ya kuvutia ili kutangaza na kukaribisha watalii visiwani.

Katika mbinu hiyo, wapigambizi au maarufu wapiga makachu, wanajirusha kutoka juu na kuchupa hadi baharini kwa madaha, wakibeba mabango yenye majina na picha za watu maarufu na vivutio kadhaa.

Ni pamoja na picha ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, bendera za mataifa mbalimbali na maneno ya ukaribisho mfano karibu Zanzibar ufurahie maajabu mengi.

Serikali inawasifu wapigambizi hao kwa kufanya juhudi za ziada kuiunga mkono kuitangaza Zanzibar kitaifa na kimataifa kwenye utalii. Nipashe inakutana na vijana hao eneo la Forodhani wakifanya makubwa si kutangaza utalii visiwani humu pekee lakini pia wamekwenda mbali zaidi kwa kuonesha dhamira njema kwa maendeleo ya kiuchumi kupitia kuonesha vivutio na rasilimali zilizopo.

Wanasema maendeleo ya visiwa duniani hutegemea kukuza utalii, ujenzi wa hoteli za nyota tatu hadi tano, mvuto wa fukwe za bahari na usalama wa wageni. Aidha, kukua kwa utalii lazima kuendane na miundombinu hasa barabara ,viwanja vya ndege, usafiri wa ndani, umeme wa uhakika ,matibabu na maji safi na salama.



Mmoja wa wapiga makachu akionesha ujuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Hivyo kujitolea kwa vijana wapiga makachu kwenye ufukwe wa Forodhani si kwamba kumeendelea kuitangaza Zanzibar kiutalii ,lakini pia huwavutia watalii wengi wa ndani na nje kutembelea visiwani.

Endapo Wizara ya Utalii Zanzibar moja ya kazi yake ni kufanya matangazo ya kuutangaza utalii kimataifa, basi wapiga makachu wamechemsha bongo zaidi na kuibua ajira hivyo wanastahili kulipwa na kuheshimika.

Kazi kubwa imekuwa ikifanywa na vijana hao ya kujirekodi huku wakiwa hewani na kuchupa baharini wakipiga mbizi kwa madaha, mitindo mbalimbali wakiwa na mabango.

"Karibu Zanzibar, Zanzibar hakuna matata, Zanzibar ni njema atakaye aje, njoo Zanzibar ucheze na sisi, au uogelee na pomboo."

Zanzibar au Unguja na Pemba hakuna madini ya kutosha lakini rasilimali zake chini ya bahari zinaweza kuendesha maisha ya wananchi ikiwa zitatumika kwa haki, usawa na uwazi, wanasema.

Bahari yake yenye samaki wengi wa aina mbalimbali, misitu yake midogo ya Jozani na Ngezi inawavutia watalii wengi na watafiti wa tiba na dawa za miti.

Kuna mtandao wa barabara kutoka Unguja zinazofika maeneo yote ya kaskazini mashariki na kusini ambako ndiko kwenye hoteli kubwa za kitalii na zaidi bado zipo fursa nyingi ambazo zikitumika kikamilifu zinaweza kubadili mfumo wa maisha kwa Wazanzibari na kuanza kuishi kwa ubora zaidi.

**MWINYI AWATAMBUA**

Rais Dk Mwinyi anasema wapiga makachu wameiheshimisha Zanzibar kwa sababu kazi wanayoifanya inaonekana dunia nzima kwa kulitangaza taifa na uzuri wake.

Anasema hatua hiyo ya vijana kwa ubunifu bila shaka imeongeza idadi ya watalii wanaofika Zanzibar.

"Video zenu zimesambaa dunia nzima na nimekuwa napokea ujumbe mbalimbali wa pongezi kutokana na kazi yenu mnayoifanya ya kuitangaza nchi hongereni sana vijana wangu"anasema Dk. Mwinyi.

Zanzibar imefungua milango wazi kwa fursa za biashara na uwekezaji na tayari imewakaribisha wadau mbalimbali kushirikiana nao kwenye maono ya ukuaji wa uchumi endelevu na ustawi wa utalii wa muda mrefu.

Hatua hiyo, itaiwezesha Zanzibar kuwa kituo bora cha ushindani kwa utalii kwenye ramani ya dunia, anasema Rais Mwinyi.

Utalii wa Zanzibar umejikita zaidi katika fukwe hivyo ni vyema kuwekeza katika utalii mwingine ikiwemo wa michezo na uwekezaji, aidha Rais Dk. Dk.Mwinyi anajivunia miaka minne ya uongozi wake akiona kwamba sekta ya utalii inapiga hatua kubwa na kuwa uti wa mgongo wa uchumi huku ikichochea uwekezaji wa miradi mbali mbali kwa vijana.

"Utalii unaendelea kuwa tegemeo la kukuza uchumi na uwekezaji ambapo naahidi mazingira mazuri yanaimarishwa na kuona Zanzibar inakuwa kituo bora Afrika katika utalii." Anasema Rais.

Kadhalika, kwa mujibu wa Rais Zanzibar imefungua milango katika fursa za biashara na uwekezaji ambapo sekta hiyo imepata mafanikio kufuata kujitangaza duniani kote.

Aidha, anaahidi kuhakikisha hakuna vikwazo vitakavyokwamisha maendeleo ya sekta hiyo ambayo inachangia ajira kwa vijana akiongeza.

**INAENDELEA UK.12**

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Chumvi ni bora lakini ni hatari zaidi

CHUMVI hufanya chakula kuwa na ladha. Pia ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu. 'Madini ya 'sodiamu' yaliyoko katika chumvi ni muhimu kudumisha kiwango sahihi cha maji mwilini. Pia huwezesha seli kunyonya virutubisho.

"Chumvi ni muhimu katika maisha," anaeleza Paul Breslin, profesa wa sayansi ya lishe katika Chuo Kikuu cha Rutgers nchini Marekani.

"Chumvi ni muhimu sana kwa seli za binadamu , ikijumuisha nyuroni au mishipa ya fahamu yote , ubongo, mgongo na misuli yetu yote. Pia ni muhimu kwa ngozi na mifupa."

Lakini , Profesa Breslin anaonya, ikiwa hatuna sodiamu ya kutosha tutakufa maana seli na mishipa ya fahamu haiwezi kufanya michakato yake. Upungufu wa sodiamu mwilini husababisha kuchanganyikiwa, hasira, misuli kutofanya kazi vizuri, kukakamaa na hata koma au kiharusi.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linapendekeza kula chumvi kiasi cha gramu tano kila siku yenye gramu mbili za sodiamu.

Lakini wastani wa kula chumvi kimataifa ni karibu gramu 11 kwa siku. Hilo huongeza hatari ya magonjwa ya moyo na mishipa, saratani ya tumbo, unene, maradhi ya mifupa na ugonjwa wa figo. WHO inakadiria watu milioni 1.89 hufa kila mwaka kutokana na matumizi ya chumvi kupita kiasi.

Katika nchi nyingi, matumizi ya chumvi kupita kiasi hutokana na kiasi kilichofichwa katika vyakula vilivyochakatwa.

Watu wa Kazakhstan hutumia karibu gramu 17 za chumvi kwa siku, zaidi ya mara tatu ya kiasi kilichopendekezwa na WHO.



Ukiongeza chumvi chakula kinakuwa kitamu zaidi lakini ni hatari. Unapaswa kuacha kuiongeza chumvi mbichi mezani kwenye mlo. Weka kiasi kidogo halafu ipikwe. **PICHA: MTANDAO**

Maryam anaishi Astana, ambao ni mji mkuu wa Kazakhstan, anataja sababu za kula chumvi kwa wingi, : "Ni kutokana na urithi wetu. Kwa karne nyingi tulizunguka misituni, tukiwa na nyama ambazo zilipaswa kuhifadhiwa kwa kutumia chumvi."

"Familia zilihifadhi nyama kwa msimu wa baridi. Wanaweza kuhifadhi ng'ombe mzima, kondoo na hata nusu farasi."

Miaka minane iliyopita, binti wa Maryam alikuwa na matatizo ya kiafya. Daktari wake alimshauri apunguze vyakula vyenye sukari nyingi, mafuta na chumvi kwa wingi. Familia iliacha mara moja kuongeza chumvi kwenye chakula chao. Na hatimaye Mariyam na jamaa zake walizoea maisha bila kuongezwa chumvi.

Unapokula chumvi, ladha yake unaihisi kwenye ulimi na kaakaa laini la koo.

"Chumvi hutia nguvu mwili na akili pia," anasema Profesa Breslin.

Sodiamu huyeyuka kwenye mate. Kisha huingia kwenye seli za ladha na kuamsha seli moja kwa moja.

"Chumvi hupeleka mawimbi ya umeme ambayo huamsha mawazo na hisia. Kwa hivyo mwili na akili zetu huchangamka." Anaongeza.

Athari ya chumvi kwenye mwili inategemea muundo wa vinasaba wa mtu. Zaidi ya watu bilioni moja duniani kote wanakabiliwa na shinikizo la damu. Kupunguza ulaji wa chumvi kunaweza kusaidia kuzuia hilo na kutibu tatizo hilo linalosababisha koma au kiharusi wakati mwingine.

"Unapokuwa na chumvi nyingi, jambo la kwanza ambalo mwili wako hufanya ni kuiyeyusha. Kwa hivyo shinikizo la damu hupanda ili kusukuma maji ya ziada," anaeleza Claire Collins, profesa wa lishe na milo katika Chuo Kikuu cha Newcastle nchini Australia.

"Ikiwa una udhaifu wowote katika mishipa yako ya damu, kama ile ya ubongo, inaweza kupasuka na kusababisha kiharusi."

Nchini Uingereza, wastani wa matumizi ya chumvi umepungua hadi gramu nane kwa siku, ambayo bado ni zaidi ya viwango vilivyopendekezwa. Upunguzaji huo unatokana na kanuni walizowekewa watengenezaji wa chakula kupunguza viwango vya chumvi.

Ulaji wa chumvi unaopendekezwa hutofautiana kutoka nchi hadi nchi. Kipimo cha mkojo kinaweza kugundua ikiwa mwili wako una chumvi nyingi au kidogo.

### KUIPUNGUZA

Hata kama kiwango chako cha chumvi ni cha juu, kupunguza kunaweza kuwa sio rahisi sana. Lakini Prof Collins anahimiza kula mkate au tambi au chakula kingine chochote ambacho kina kiwango cha chini cha chumvi.

"Ikiwa unapika chakula chako mwenyewe weka mitishamba na viungo badala ya chumvi." Anasisitiza. Ni maelezo ya BBC Swahili.

### CHUMVI NI UHAI

Kwa upande wa mitandao mingine, wanyama wote wenye damu moto, lazima wale chumvi ili kuishi. Ubongo wa binadamu pamoja na uti wa mgongo, vimo katika mfuko wa maji chumvi uitwao 'cerebrospinal fluid (csf)'. Umajimaji huu huzunguka sehemu zote za ubongo na uti wa mgongo.

Machozi ni chumvi na jasho pia ambalo pia ni chumvi. Mifupa ina uwazi katikati yake au uroto ambamo seli za damu hutengenezwa. Uroto umefunikwa na tabaka nyingi za chumvi kalisiamu kama vile kamba inavyoshikizwa pamoja. 'salt crystals' au chenga chenga za chumvi, zinashikizwa pamoja na kalisiamu, na ndizo zinazoifanya mifupa kuwa imara, na siyo kalisiamu pekee.

Mifupa inamiliki asilimia 27 ya chumvi yote mwilini. Wakati mwili unahitaji chumvi zaidi, huikopa toka mifupani, jambo hili likitokea, kalisiamu huondolewa pamoja na chumvi na kuifanya mifupa kuwa miembamba, laini na midhaifu.

Chumvi imeundwa kwa sodiamu na klorini, kwa pamoja inaitwa; 'sodiamu kloraidi'

### VYAKULA NA CHUMVI

Wakazi wa ukanda wa pwani kuanzia Tanga hadi Mtwara huhifadhi vyakula kwa chumvi tena huwekwa nyingi ,mfano ni dagaa, nyama, papa na nguru pamoja na samaki kutoka Morogoro wanaokaangwa na kujazwa chumvi.

## Z'bar yapaa kiutalii; chanzo ubunifu, video za wapiga makachu zatikisa duniani

INATOKA UK.11

"Katika miaka minne tumeupa utalii kipaumbele kuona unachangia pato la taifa na kukuza uchumi sambamba na uwekezaji, unaozalisha ajira kwa vijana."

"Nilipoingia madarakani niliahidi kufanya kazi na sekta binafsi kuendesha nchi na leo mafanikio tunayaona katika upande wa utalii ambapo wenzetu wanafanya kazi vizuri na serikali".

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, anasema sekta ya hiyo inapiga hatua na katika mwaka wa fedha 2024-2025 wataimarisha utalii wa majengo ya kale na kutangaza vivutio viliopo.

Anayataja mafanikio makubwa ya kuimarika kwa sekta ya utalii ikiwemo kuwepo kwa amani na utulivu ambao ndiyo dira itakayowafanya watalii kuendelea kuja Zanzibar.

"Katika kipindi cha miaka minne tumeimarisha sekta ya utalii na kufungua milango ya kuitangaza nje na miongoni mwa mambo yaliyowavutia wageni ni kuimarika kwa amani na utulivu,"anasema.

Waziri Soraga, anaongeza kuwa serikali ikichukua jitihada mbalimbali kuhakikisha inaweka mazingira bora na wezeshi kuinua sekta hiyo ambayo ina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

"Tutaendelea kushirikiana na wadau kupeleka ajenda ya kukuza utalii mbele ili Zanzibar iwe mfano katika eneo hili," anaahidi.

Hivyo anawakaribisha wadau kuwekeza Zanzibar kwasababu ambayo ni salama kwa mitaji na biashara zao na kwamba miaka minne imeakisi maendeleo endelevu ya sekta hiyo na kukuza biashara na maendeleo hivyo matarajio yake huduma zitaongezeka.

Akilizungumzia eneo la Forodhani kwa wapigaji makachu, anasema ni kivutio kikubwa kuendelea kutangaza Zanzibar kwa sababu utalii ni muhimu.

Mmoja wa wapiga makachu Hassan Othman, anasema ni furaha kwao kuona jambo wanalolifanya linathaminiwa na kuonekana katika mataifa mbalimbali dunianina kuchangia kukuza utalii.


Anasema imekuwa fursa kwa vijana kupata ajira kwa sababu hupata fedha wanazotunzwa na watalii mbalimbali.

Albaina Ally ni mwanamke wa kwanza kuruka makachu katika eneo hilo la Forodhani anasema baada ya kuona umchezo huo ukifanywa na wanaume pekee alishawishika na yeye kushiriki ili wanawake nao wasiachwe nyuma katika fursa mbalimbali ikiwemo za utalii.

"Mwanzo ilikuwa ngumu lakini nikasema ngoja nijaribu, siku ya kwanza nilishindwa kutokana na mazingira ya eneo lenyewe lakini vijana wanaume Forodhani wakaniunga mkono na uthubutu wangu umevuta wanawake wengi kujikita katika mchezo huu,"anasema.

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere kinavyolenga kuwa gwiji KITEHAMA



Makamu Mkuu wa Chuo cha MJNUAT, Profesa Lesakit Mellau na mwakilishi wa kampuni itakayoboresha miundombinu ya chuo, Li Manchao, wakisaini mkataba. **NA MPIGAPICHA WETU**

DUNIA ya sasa kila jambo linafanyika kielektroniki likipewa nguvu na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Teknolojia hiyo inahusisha zana na nyenzo za kiufundi zinazotumiwa kuunda, kuhifadhi, kushiriki (share) na kusambaza taarifa ambazo hutegemea kompyuta, mitandao, programu, intaneti, simu za mkononi na mikutano ya video

Zama hizi TEHAMA ni kila kitu anatumiwa karibu kwenye kila eneo, shuleni hadi vyuoni viwe vya kati hadi vikuu. Tiba, usafiri, kilimo, viwandani na utoaji wa huduma.

Pia TEHAMA inarahisisha shughuli za masomo ikiwamo kufundisha na kujifunza. Kutokana na umuhimu wa teknolojia hiyo, Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) kilichoko Mara kiko mbioni kujenga Shule Kuu ya TEHAMA katika kampasi zake.

Shule hizo za TEHAMA zinatarajiwa kujengwa kampasi kuu ya Butiama na Tabora ikiwa ni sehemu ya mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya MJNUAT.

Katika ziara ya kutembelea na kukagua ujenzi wa mindombinu ya MJNUAT, Makamu Mkuu wa chuo, Profesa Lesakit Mellau, hivi karibuni anaueleza ujumbe wa baraza la chuo, unaozuru chuo kikuu kuwa wameingia mkataba wa ujenzi wa shule hizo.

Anawafafanulia wajumbe wanaoongozwa na Profesa Roberta Malee wa Benki ya Dunia(WB), aliyeambatana na wadau wengine wa elimu wakiwamo wengine kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Chuo kimepata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mchanganyiko katika kampasi kuu Butiama na kusaini mkataba wa miezi 10 na kampuni ya China kukamilisha kazi hiyo, " Profesa Mellau anasema.

Anaongeza kuwa mkataba huo wenye thamani ya Sh. bilioni tisa ulifanyika katika kampasi kuu Butiama na kushuhudiwa na watu mbalimbali akiwamo Mkuu wa mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi na mwenyekiti wa baraza la chuo hicho, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu Philemon Luhanjo.

Anafafanua kuwa mkataba huo utahusisha ujenzi wa barabara za ndani ya chuo, mifumo ya majitaka na ya kusambaza maji safi, lango kuu la chuo, sehemu ya kuweka taka na tanuru la kuzichoma na miundombinu ya michezo.

Vilevile, wiki iliyopita chuo kiliingia mkataba wa ujenzi wa Shule Kuu ya TEHAMA na biashara katika kampasi za Tabora na Butiama chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) , mkopo kutoka Benki ya Dunia kwenda serikalini.

Aidha, anasema chuo kimeanza kupokea wanafunzi wa mwaka wa kwanza tangu mwezi uliopita ( kuanzia Oktoba 30).

Profesa Mellau anasema ujenzi wa chuo utakapokamilika, kitadahili wanafunzi hadi 4,500 kwa kampasi kuu, 600 katika kampasi ya Oswald Mang'ombe na wanafunzi 1,500 kwa kampasi ya Tabora na kinatarajiwa kuwa na watumishi 700.

"Tunashirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, Benki ya Dunia na taasisi nyingine za elimu ya juu kuusimamia mradi huu ili ukamilike kwa wakati," anasema.

Anaongeza kuwa chuo hicho ni miongoni mwa taasisi 23 zinazonufaika na Mradi HEET ambao ni mkopo kutoka WB kwa serikali.

## MAADILI MEMA

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha MJNUAT, Philemon Luhanjo, anawataka watumishi wa chuo hicho kuzingatia maadili mema.

Anasema hayo wakati akizungumza na wanataaluma wa chuo hicho, katika kampasi ya Oswald Mang'ombe, Butiama kwenye ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya MJNUAT.

Luhanjo anasema kilianzishwa ili kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na kwamba maadili ni jambo la muhimu kwa watumishi na wanafunzi wa chuo hicho.

"Ni lazima tuonyeshe taswira inayofanana na Mwalimu Nyerere. Chuo hiki ni maalumu na kimekuja kuwekwa katika kijiji chake. Muitunze heshima ya Mwalimu Nyerere," anasema Luhanjo.

Katibu Mkuu kiongozi mstaafu anasema ni muhimu kulinda taswira ya chuo hicho na kuepusha mazingira yatakayowafanya watu wakiseme vibaya.

"Sisi tujitahidi kukijenga na kukiimarisha ili tuweze kutengeneza taswira ile inayotakiwa au zaidi. Kwa hiyo suala la maadili, kwa maana pana - ninyi wenyewe (watumishi), wanafunzi kwa wanafunzi, walimu kwa wanafunzi, walimu na wanafunzi na jamii inayowazunguka, muwe na mahusiano mazuri," anasema.

> Ni lazima tuonyeshe taswira inayofanana na Mwalimu Nyerere. Chuo hiki ni maalumu na kimekuja kuwekwa katika kijiji chake. Muitunze heshima ya Mwalimu Nyerere.

## FURSA KEDEKEDE

Mkuu wa Mkoa wa Mara Kanali Evans Mtambi anasema uwepo wa chuo hicho Butiama, umeleta fursa nyingi za uwekezaji na kuwataka wakazi wa mkoa huo na maeneo mengine kuchangamikia fursa hiyo.

"Niwaombe wananchi wa mkoa wa Mara na Watanzania kuchangamkia fursa ya kuanzishwa kwa chuo hiki kuwekeza katika biashara mbalimbali zitakazokuwa zinahitajika kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi na watumishi," anasema Kanali Mtambi.

Kanali Mtambi anafafanua kuwa wawekezaji wanaweza kufungua maduka kulingana na mahitaji ya wanafunzi, watumishi wa chuo na watu wengine wanaoishi maeneo ya jirani na chuo.

Aidha, uamuzi wa serikali kukifanya chuo hicho kibebe sehemu ya kumbukumbu ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, imewekeza fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wake ili kuleta mapinduzi makubwa ya kijamii na kiuchumi katika mkoa huo.

"Chuo hiki kinasadifu shabaha halisi ya kumuenzi Baba wa Taifa, mkoa wetu tunaishukuru serikali kwa maamuzi haya ya ya kujenga chuo hiki mkoani Mara ukiwa mmoja kati ya miradi mikubwa kitaifa," anasema.

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

BAADA YA KIFAA MOYONI...

# Ni zamu ya kukipachika ubongoni usahaulifu huenda ukawa historia

KAMA moyo unavyowekewa kifaa kuuponya ili usukume damu kwa kasi inayohitajika sasa ni zamu ya ubongo kupachikwa vifaa vya 'kuubusti' pale unapoanza kuchoka na kushindwa kazi.

Lakini tiba ya vifaa si moyoni pekee kinapobandikwa kudhibiti matatizo hata sikio huwekewa kisaidizi kiitwacho 'cochlear' kuboresha usikivu.

Yote hayo yamefanikisha maisha ya mamilioni ya watu kubadilishwa kwa kupandikizwa vifaa vidogo vya kielektroniki vinavyoongeza ufanisi.

Mambo yanazidi kusonga mbele sasa timu ya Cambridge nchini Uingereza kutoka sekta ya afya, sayansi na biashara imepewa mamilioni ya dola kugundua kwa haraka teknolojia mpya zinazolenga kuboresha afya na ufanisi wa ubongo.

Watafiti wa Uingereza watapewa fursa za kufanya majaribio. Watatumia matokeo ya kutibu watu wanaougua shida ya akili, unyogovu au depression na maumivu sugu kama usahaulifu.

Profesa George Mellieras, mmoja wa wanasayansi wakuu kwenye timu ya Cambridge, anatumaini tangazo hilo litasaidia mradi wake mpya.

**KUGUSA UBONGO**


Teknolojia ya kusaidia kutibu matatizo ya afya ya akili, inayofanyika Chuo Kikuu cha Cambridge inakadiria kuwa baadhi ya matatizo ya neva au mishipa ya fahamu au akili huathiri watu wanne kati ya watano.

Timu ya Profesa George Melliaras inatafiti vifaa vidogo ambavyo vinaweza kusaidia kutoa matibabu, akisema.

"Vipandikizi vya ubongo vinaweza kutoa tiba mpya ya magonjwa ambayo hayawezi kutibiwa kwa dawa,"

"Orodha ya magonjwa ya aina hiyo inaendelea na kuendelea. Lakini tunachozungumzia hapa ni majeraha ya ubongo na uti wa mgongo kama parkinson's amnesia ambayo ni usahaulifu na kutetemeka pia kuna depression au unyogovu.

Kadhalika lipo tatizo la obsessive-compulsive disorder ambayo ni matatizo ya akili ambayo huleta kuhisi haja ya kuangalia kitu kimoja mara kwa mara, kufuata utaratibu fulani mara zote, au kuwa na mawazo yaleyale muda wote.



Kifaa saidizi cha moyo 'heart pacemaker' kinachotumika kuongeza ufanisi kwenye moyo unaposhindwa kazi ya kusukuma damu mwilini ipasavyo. **PICHA: MTANDAO**

> Elektrodi zinazotoka kwenye kifaa hiki hazipaswi kuwa kubwa kuliko nyuroni moja. Ukubwa huu ni mdogo mara tano kuliko kipenyo cha nywele za binadamu.



Kadhalika maradhi kama 'rheumatoid arthritis' ambayo husababisha kuvimba viungo, misuli, mishipa na mifupa, vifaa hivyo vinatarajiwa kusaidia kutibu aina ya kwanza ya kisukari ambayo mtoto huzaliwa na shida kwenye tezi kongosho ambalo halizalishi insulin na kuchakata sukari kwenye damu ili kupata nishati ya kufanyakazi," anasema.

Wenye aina ya kwanza ya kisukari hutumia sindano ya insulin muda wote ili kujipa kichocheo hicho kinachobadilisha sukari kuwa nishati au nguvu ili mwili ufanyekazi.

Pia anaongeza kuwa ni utafiti unaofaa na wa kutia moyo sana.

Mabadiliko katika namna neva zinavyofanya kazi yanaelezwa kuwa vifaa hivyo vilivyopandikizwa mwilini hutuma mawimbi madogo madogo ya umeme ili kubadilisha jinsi nyuroni katika miili inavyofanya kazi.

Seli za neva zinazoitwa nyuroni husambaza ujumbe kati ya mwili na ubongo kupitia msukumo wa umeme.

Aidha, zinadhibiti mwelekeo wa kutembea, kuzungumza, kula na kupumua. Watafiti wanaamini kwamba kwa kubadilisha jinsi nyuroni hizo zinavyofanya kazi, inawezekana kupunguza maumivu au kuchochea tena maeneo yaliyoathirika ya ubongo.

"Tayari tunajua kuwa kutumia kichocheo cha umeme kunaweza kupunguza kutetemeka kwa baadhi ya watu wenye kifafa," anasema Profesa Melliaras.

Anaongeza, "Lakini ili kuendeleza aina hii ya teknolojia tunahitaji kuleta pamoja timu ya wahandisi, madaktari na viwanda kote Uingereza."

**CHANGAMOTO**

Ukubwa wa chombo hiki ni changamoto kwa watafiti.

"Elektrodi zinazotoka kwenye kifaa hiki hazipaswi kuwa kubwa kuliko nyuroni moja. Ukubwa huu ni mdogo mara tano kuliko kipenyo cha nywele za binadamu, " anataja Profesa Melliaras.

"Lakini kifaa kikiwa kidogo sana, kitakuwa na matatizo katika kuwasiliana na mwili. Madaktari wanaweza kupata ugumu wa kukipandikiza kwenye mwili wa mgonjwa. Kinapaswa kuwa suluhisho la matatizo yote mawili kwa usawa," aliongeza.

Pia, lazima wahakikishe kuwa kifaa cha kuingiza sauti kimezalishwa kwa wingi, kwa gharama nafuu, na hakina madhara kwa wagonjwa.

Vipandikizi vya matibabu si vipya kwa wahandisi hawa. Dk. Chaukun Tong anatengeneza kifaa ambacho hufunika mishipa dhaifu bila kuiharibu.

Dong anatafiti nyenzo ambayo inaonekana kama utepe mdogo kwenye kiputo cha kioo. Imetengenezwa kwa polima iliyowekwa dhahabu.

Wakati umeme unatumika, hujikunja kwa hiari. Vifaa hivi husaidia kufuatilia ishara za msukumo kutoka kwa neva na kuzichochea wakati wa upasuaji tata.

Umeme umetumika kwa muda mrefu kutibu magonjwa mengi. Tiba ya electroconvulsive (ECT) kama matibabu ya msongo mkubwa na ugonjwa wa mshtuko wa moyo ilianza miaka mingi iliyopita, lakini Melliaras anaamini kwamba, ingawa utaratibu wa upasuaji utafuatwa ili kuweka vifaa vya kupandikiza, itakuwa na manufaa kama matibabu ya mara moja kwa magonjwa huyo.

Vifaa vinavyoweza kupandikizwa vinaweza kugundua shughuli isiyo ya kawaida kwa kufuatilia ubongo kila mara na kurekebisha kwa upole inapohitajika, anasema.

Matokeo ya utafiti uliochapishwa na wanasayansi wa Marekani mwaka 2021 yalikuwa na matumaini kwamba suluhu inaweza kupatikana kwa kupandikiza vifaa vya kuingiza kwenye ubongo ili kutibu uchovu mkubwa wa kiakili.

Profesa Melliaras ana uhakika kwamba ndani ya kipindi hiki, wataweza kufika mbali katika kutafiti tiba mpya ya kuweka kifaa ubongoni. **BBC**





## Jamii yatakiwa kuwajenga watoto kwenye misingi bora

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Taasisi ya Fountain Gate Foundation, Japheth Makau, amesema jamii inapaswa kuwajenga watoto kwenye misingi ya kuwa na kiasi ili kuondoa kizazi chenye tamaa ya kujilimbikizia mali na kushindwa kusaidia wenye uhitaji wakiwemo yatima na maskini.

Alitoa rai hiyo juzi jijini hapa, wakati wa tukio la mwaka la taasisi hiyo la kusaidia wenye uhitaji ambapo misaada mbalimbali ilitolewa kwa wanafunzi wa Shule ya Buigiri pamoja na kituo cha makao ya taifa ya kulelea watoto Kikombo.

Alisema siku hiyo ni maalumu kwa ajili ya kurudisha kwa jamii ambapo misaada mbalimbali imetolewa kwa wenye uhitaji ikiwemo vyakula, mavazi pamoja na kushiriki michezo na chakula kwa pamoja.

"Tumefanya shughuli hii kwa miaka 10 sasa na Mungu ameendelea kutubariki pale tulipotoa hatujapungukiwa hii kwetu ni ibada kubwa sana ambayo tunaifanya tulianza miaka kadhaa iliyopita.

Meneja wa taasisi hiyo, Paul Mganda alisema wanazo programu kuu nne ambazo ni elimu na vipaji ambapo inahusisha ufadhili wa kimasomo kwa watoto wenye uhitaji na wenye historia ya kipekee.

Alisema wanao watoto wanaoishi katika mazingira magumu wakiwemo yatima na waliotelekezwa na familia zao ambao wanafadhiliwa kwa kuendelezwa vipaji vyao vya kimichezo, sanaa na elimu.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Mashirika yasiyo ya kiserikali Wilaya ya Dodoma (Ngonedo), Edward Mbogo, alisema wataendelea kushirikiana na taasisi hiyo kuandika miradi ili kuhudumia jamii na kufika pale ambapo serikali haijafika.

# Biteko atahadharisha makundi kuelekea uchaguzi s/mitaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuepuka makundi endapo wanahitaji ushindi wa kishindo kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Alitoa rai hiyo juzi jijini hapa akizungumza na wanachama wa CCM kwenye mkutano mkuu wa Jimbo la Dodoma Mjini.

Alisema kama CCM inahitaji ushindi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025, wanachama wanapaswa kuvunja makundi yao na kuwa kitu kimoja kukipigania chama.

"Kama tunahitaji kushinda ni lazima kuwa kitu kimoja kufanya kazi kwa ushirikiano tutofautiane katika vikao vyetu vya ndani lakini tukitoa nje tuwe kitu kimoja kwa ajili kukipigania chama chetu kushinda kwenye chaguzi hizo" alisema Dk. Biteko.

Aidha, alisema anaimani kuwa CCM itafanya vizuri kwenye chaguzi zote hizo kutokana na maandalizi yanayoendelea kufanyika.

"Sioni kama kuna chama kingine ambacho kimejiandaa kama ilivyo kwa CCM, lakini pia licha ya maandalizi hayo pia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi uliofanywa na chama chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan vinatosha kabisa kukipa ushindi wa kishindo chama chetu" alisema.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi katika Jimbo la Dodoma kwa kipindi cha miaka minne Mbunge wa Dodoma na Waziri wa Madini, Antony Mavunde alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana lakini bado zipo changamoto mbalimbali.

Alisema moja ya changamoto hizo ni pamoja na migogoro ya ardhi na uhaba wa maji hali ambayo inahitaji jitihada za makusudi kuzikabili.

Alisema katika kipindi cha miaka minne wamepokea Sh. trilioni 1.5 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika jimbo la Dodoma Mjini.

Alisema fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, barabarani ya mzunguko kilomita 112.3, ujenzi wa Uwanja wa Maonyesho ya Nanenane ya Kudumu na Mji wa Serikali Mtumba.

Alitaja miradi mwingine ni ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu, ujenzi wa chuo cha ufundi, soko la kisasa la machinga, ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati, ujenzi wa shule za sekondari na msingi na ujenzi wa miradi ya maji.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati alipofunga Mkutano wa Kazi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Baraza la Mawaziri (e-CABINET), kwenye ukumbi wa Hazina jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Tembo wavunja nyumba 15, kula chakula

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

WANANCHI wa Kijiji cha Gurungu, Kata ya Sanjaranda Halmashauri ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida wameanza kukimbia makazi baada ya tembo kuvamia makazi yao, kuvunja nyumba na kula mazao yaliyokuwa yamehifadhiwa.

Diwani wa Kata ya Sanjaranda, Nicodemus Msubiri, alimweleza hayo jana Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alipotembelea na kuzungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Sanjaranda ambao wameanza mitihani ya kuhitimu kidato cha nne.

Alisema tembo hao walivamia kijiji hicho mwishoni mwa wiki, baadhi ya wananchi wameanza kuhamia vijiji jirani ili kunusuru maisha yao.

Msubiri alisema hatua zilizochukuliwa kwa sasa ni wametoa taarifa kwa askari 18 wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ambao wameweka kambi katika Kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kashangu walimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa hali ni mbaya kijijini hapo kwamba kila mara tembo wamekuwa wakivamia mashamba.

"Wananchi tunashindwa kulima sababu ya tembo ambao pia wanavunja nyumba zetu, tunaomba serikali iwe inatulipa fidia kwa wakati kwani hali ni mbaya," alisema Dinno Brezi mkazi wa Kijiji cha Kashangu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dendego aliwataka wananchi ambao wameathiriwa na tembo kwenda kujiandikisha kwa maofisa watendaji wa kata ili wafanyiwe tathimini na kulipwa fidia.

Aidha aliwataka askari wa TAWA kufanya operesheni maalumu ya kuwaondoa tembo hao kwani serikali imetoa vibali na vifaa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Kumekuwa na mfululizo wa matukio ya tembo kuvamia makazi ya watu na kubomoa nyumba ambapo hivi karibuni tembo zaidi ya 56 walivamia Kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi mkoani Singida na kuvunja nyumba nane na kula vyakula majumbani.

Kufuatia tukio hilo, wananchi wa kijiji hicho walifunga Barabara ya Dodoma-Singida hali iliyomlazimu Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi, Dk. Pindi Chana, kufika katika kijiji hicho na kuagiza askari wa TAWA kuweka kambi ili kuwadhibiti tembo hao.



# Mtaka ahamasisha ushiriki upigaji kura

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ametoa rai kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ili kuchagua viongozi wanaowataka.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ukalawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

"Nawaomba wananchi wa Mkoa wa Njombe mjitokeze kwa wingi wakati wa zoezi la kuchagua viongozi kwenye kupiga kura Novemba 27 na tuone mafuriko ya wananchi wanaenda kuchagua viongozi watakaosimamia maendeleo yao kwenye vijiji vyao, kwenye vitongoji vyao na mitaa yao," alisema Mtaka.

Mtaka aliwasisitiza wananchi kuchagua viongozi bora ambao watawaletea maendeleo na hivyo kuepukana na watu wa migogoro ambao wanakuwa madalali wa ardhi za vijiji.

"Mkachague viongozi bora na siyo bora viongozi, watu ambao watafanya mambo ambayo hapa hamuyafanyi, mambo ya maendeleo naomba jitokezeni kwa wingi mchague viongozi mnaowataka kwenye mamlaka ya serikali za mitaa," alisema Mtaka.

Mtaka alisema katika zoezi la kuandikisha watu wamefanikiwa kwa asilimia 86 na kwamba matarajio yao ni kupata asilimia 100 ya watu wote waliojiandikisha kwenda kupiga kura.

Kwa upande wake, Katibu wa Itikadi, Siasa, Uenezi na Mfunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga alisema kuelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wanahitaji viongozi watokane na CCM kwa sababu ndiyo chama chenye Dira ya Maendeleo ya Taifa.

"Rais anatokana na chama chetu, wabunge, madiwani, wenyeviti wa vijiji na serikali zao, vitongoji watokane na chama cha mapinduzi ili kuweka mnyororo mzuri wa kutekeleza shughuli za maendeleo katika maeneo yetu," alisema Luoga.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Ukalawa akiwemo, Kalista Mheche alisema watakwenda kupiga kura ili kuweza kuchagua viongozi bora ambao watawaletea maendeleo.

## Waliopata ujauzito shuleni, kurejea watoa ahadi

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WANAFUNZI wa kidato cha nne waliopata ujauzito wakiwa shuleni na kurejea wameishukuru serikali kwa kuwapa nafasi nyingine, huku wakiahidi kufanya vizuri na kufaulu katika mitihani yao.

Walitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki wakati wakizungumza na waandishi wa habari katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ulembwe kilichopo wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe.

Walisema fursa ya kurejea masomoni kupitia programu maalumu kwa wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo mimba imebadili historia ya maisha yao kwa sababu ya kurudi shule na kuendelea na masomo yao.

Mmoja wa wanafunzi hao akiwemo, Devotha Lowiso alisema ameona mwanga kwa kufikia ndoto zake tena baada ya serikali kuwapa fursa ya kurudi shule baada ya kujifungua.

"Nilimaliza shule ya msingi, nikafaulu kwenda kidato cha kwanza nikasoma mpaka kidato cha pili nikamaliza nilivyomaliza nikafaulu na nilivyofika kidato cha nne mwanzoni nikashindwa kuendelea na masomo yangu kwa sababu ya changamoto ya ujauzito," alisema Devotha.


"Nina ndoto nitaendelea kusoma kwa bidi, naamini Rais Samia ameleta hii fursa kwa ajili ya watoto waliokatisha masomo iwasaidie kutimiza ndoto zao," alisema Devotha.

Naye Qeen Mbande alisema alisoma sekondari, baada ya kutoka matokeo ya kidato cha pili alifaulu lakini alishindwa kuendelea na masomo kutokana na ugumu wa maisha wa familia yake.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ulembwe, Johanes Chongoli alisema programu hiyo ilianzishwa mwaka 2022 na kutoa fursa kwa wanafunzi waliopata ujauzito na kujifungua kupata masomo ya sekondari na ufundi stadi jambo ambalo limerejesha tena matumaini yao.

Alisema Rais Samia alikuja na kanuni mpya kwamba katika elimu ya sekondari ni lazima watoto watimize malengo yao tofauti na awali ilikuwa ni ufundi ili wakajiajiri.

Alisema: "Kwa hiyo hii ni hatua ya zaidi kwa sababu huyu huyu anayesoma elimu ya sekondari siyo kwamba anasoma sekondari tu anapewa mwanya wa kusoma somo la ufundi kwa hiyo anatoka na vitu viwili kwa wakati mmoja".




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akiwa katika ukaguzi wa kawaida eneo la Mvomero mkoani Morogoro jana ili kuhakikisha madereva wanafuata sheria za usalama barabarani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wazazi, walezi watakiwa kuzingatia lishe kwa watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZAZI na walezi katika Kijiji cha Luponde Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, wametakiwa kuzingatia elimu ya lishe kwa kutenga muda wa kuwahudumia watoto wao, licha ya kujikita kwenye shughuli za kujitafutia kipato.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuruthum Sadick wakati akizungumza na wananchi wa kijiji hicho.

"Tujitahidi kuwa na muda kamili wa kuwahudumia watoto, tukifundishwa tukayachukua halafu tusiyazingatie itakuwa ni kazi bure, kazi tufanye lakini tupate muda wa kuhudumia watoto," alisema Kuruthum.

Aliongeza: "Niwaombe wamama wa Njombe, ninaelewa ni watafutaji kwelikweli,asubuhi kabla hujaenda shamba hakikisha unamuandalia mtoto wako lishe iliyo bora,"alisema.

Kuruthum alisema ili kuondokana na vitendo vya ukatili kwa watoto ni lazima mama kuwa na muda wa kuzungumza na watoto wake sambamba na kuwachunguza.

"Tunaona vitendo vibaya vinafanyika kwa watoto, mnashuhudia wenyewe watoto wanabakwa, watoto wanajisiwa, hii ni kwa sababu wamama tumewaacha watoto wetu hatuna muda nao," alisema Kuruthum.

Alisema wazazi wanapaswa kuwaangalia na kuwakagua watoto wao mara kwa mara kwa sababu malezi na kutunza familia kwa asilimia kubwa yanafanywa na mama.

Mkurugenzi huyo aliwaomba wazazi waliopatiwa elimu kufikisha elimu hiyo kwa waume zao sambamba na kuhakikisha wanakuwa na bustani ya mboga nyumbani ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa kundi la mboga kwenye mlo wa familia.

Hivyo, alimtaka mtendaji na ofisa kilimo wa kata ya Luponde kushirikiana na uongozi wa kijiji kutoa elimu ya kulima bustani jiko ili jamii yote ihamasike kupanda mboga nyumbani.

Kwa upande wao, wananchi akiwemo Mary Msigwa alisema wataizingatia elimu waliyopewa ingawa wanakabiliwa na tatizo la wanaume kuwatelekezea watoto na hivyo kulazimika muda mwingi kutafuta kipato ili kulisha familia.

"Hapa ukiangalia wanawake wengi wanahudumia familia wenyewe na muda wa kukaa na watoto kweli hakuna lakini tutajitahidi kwahudumia watoto wetu," alisema Msigwa.

Hali ya udumavu katika Halmashauri ya Mji Njombe imepungua kwa asilimia tatu kutoka 45% kipindi cha Desemba 2022 hadi 42% mwaka 2024.





## Serikali, taasisi zasaini uchunguzi, kinga ya saratani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesaini makubaliano na Taasisi ya Aegle Group ya nchini Mauritius kuwekeza kwenye uchunguzi pamoja na kinga ya saratani.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Amour Suleiman Mohammed alisema faida kubwa ya makubaliano hayo ni kujengwa kituo maalumu katika maeneo ya Binguni visiwani Zanzibar kitakachotoa matibabu ya kibingwa ya saratani.

Alisema kwa muda sasa kuna tatizo la kusafirisha wagonjwa hao Tanzania Bara na India, hivyo mkataba huo utasaidia kuondosha tatizo hilo na matibabu hayo kufanyika visiwani humo.

Alisema kuwa taasisi hiyo pia imedhamiria kuweka vifaa vya kisasa kwenye hospitali hiyo itakayoweza kugundua matatizo hayo mapema.

Aidha, aliishukuru taasisi hiyo kwa kukubali kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya katika kuimarisha huduma za matibabu hasa kwenye upande wa miundombinu, uchunguzi na kinga dhidi ya maradhi ya saratani.

Naye Mtendaji Mkuu wa Aegle Group, Dk. Vineet Kumar Singh, alisema matumaini makubwa ni kuona hospitali itakayojengwa inawanufaisha wananchi wa ndani na nje ya Zanzibar kutokana na miundombinu itakayowekwa.

Alisema kukamilika kwa hospitali hiyo ni sehemu ya kufikia huduma za afya kwa watalii wanokuja nchini.

# ZDCEA yataifisha mali za wahalifu dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, imetaifisha mali za wahalifu wa dawa za kulevya za Sh. milioni 976.

Kutaifishwa kwa mali hizo ni kwa mujibu wa Sheria ya Dawa za Kulevya Zanzibar Namba 8 ya Mwaka 2021 ambapo chini ya Kifungu cha 73 (1) kimempa uwezo kamishna wa mamlaka hiyo kufanya hivyo baada ya kujiridhisha.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamishna wa Mamlaka hiyo, Kanali Burhani Zuberi Nassoro, aliwataja wahalifu waliotaifishiwa mali zao ni Saleh Khamis Baslema, mkazi wa Chukwani, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema Aprili 22 mwaka jana mamlaka ilitaifisha mali za mtuhumiwa huyo pamoja na mkewe Gawar Bachi Fakir za Sh. bilioni 15.3 baada ya kubainika kuingiza kiasi kikubwa cha dawa za kulevya aina mbalimbali Zanzibar.

Alisema mamlaka imeendelea kufuatilia mali zake nyingine ndani ya Zanzibar na kuzitaifisha za Sh. milioni 422.1 ikiwemo kiwanja kilichopo Bweleo Mkoa wa Mjini Magharib chenye thamani ya Sh. milioni 35.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine ni Andreas Wolfgang Fretz, raia wa Ujerumani ambaye ametaifishwa mali za Sh.milioni 518.9 ambapo mtuhumiwa huyo alikamatwa Oktoba 12, 2023 majira ya saa 04:00 asubuhi baada ya kupata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa mtuhumiwa ameanzisha kilimo cha kisasa cha dawa za kulevya aina ya bangi mseto (skanka) katika Kijiji cha Paje Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema katika operesheni hiyo mtuhumiwa alikutwa na mashine ya kisasa ya kuoteshea miche ya bangi, shamba za bangi na kipolo kilochokuwa na bangi iliyovunwa tayari kwa kuifikisha sokoni.

Alisema kufuatia tukio hilo ametaifisha mali zake ambazo ni gari lenye thamani ya Sh. milioni 14.9, nyumba mbili zilizopo eneo la Paje Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema serikali imedhamiria kudhibiti na kupambana na uhalifu wa dawa za kulevya Zanzibar kwa mujibu wa sheria bila kuangalia jina, wadhifa au utaifa wa mtu.



Mjasiriamali wa samaki (kulia)akimuonesha bidhaa mteja katika Soko la Kimataifa la Samaki la Ferry Dar es Salaam jana ambapo kipande kimoja cha kukaanga huuzwa kuanzia Sh. 3,000 hadi Sh. 6,000. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Vyuo vitano kushirikiana katika elimu, utafiti, ugani

**Na Mwandishi Wetu**

VYUO vikuu vitano vimesaini makubaliano ya kushirikiana katika elimu, utafiti na ugani katika kilimo, lengo likiwa ni kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Makubaliano hayo yalifanyika jana wakati wa Kongamano la Kwanza la Afya ya Maji na Watu, ambalo lilikuwa ni tukio la kwanza la pamoja la muunganiko wa vyuo hivyo.

Vyuo vilivyoshiriki ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Afrika (NM-AIST), Chuo Kikuu cha Simon Fraser (SFU) kutoka Canada na Chuo Kikuu cha Aga Khan (AKU).

Lengo la ushirikiano huo ni kuunganisha utaalamu wao katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwa kuzingatia mazoea endelevu ya kilimo, usimamizi wa maji na afya ya umma.

Akizungumza katika kongamano hilo, Prof. Daniel Mushi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (elimu ya juu), alisema kwamba ushirikiano huo utasaidia kukabiliana na changamoto zinazoikumba Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"Wakati vyuo vinaposhirikiana, vinaweza kubadilishana maarifa na utaalamu katika maeneo ambayo baadhi ya vyuo havina uwezo au weledi wa kutosha," alisema.

Aidha, alikishukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine kwa juhudi zao za kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

Prof.Mushi alisisitiza umuhimu wa ushirikiano huo katika nchi kama Tanzania, ambapo sehemu kubwa ya watu wanategemea kilimo kama chanzo cha maisha.

"Ushirikiano huu ni muhimu katika kushughulikia changamoto za usalama wa chakula, mabadiliko ya tabianchi, na afya ya umma ambazo zinaathiri wakulima na jamii zetu kwa njia kubwa," aliongeza.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. William Anangisye, alizungumzia kuhusu maeneo mbalimbali ya ushirikiano, ikiwa ni pamoja na utafiti wa pamoja, maendeleo ya taasisi na kujengeana uwezo.

"Ushirikiano huu unalenga kukuza utafiti wa pamoja unaohusiana na njia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na tathmini ya udhaifu, ambao utanufaidha moja kwa moja idadi kubwa ya Watanzania," alisema.

Alisema ushirikiano huo unalingana na Dira ya UDSM ya Mwaka 2061, ambayo inajumuisha ahadi thabiti ya kimataifa.

"Dira yetu ni kufanya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa kitovu cha utafiti, ufundishaji, ubunifu, na kubadilishana maarifa juu ya masuala muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na kanda yetu," alisema Prof. Anangisye.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Kikuu cha Aga Khan, Zakir Mahmood, alisema kuwa mradi huo ulianzishwa mwaka jana jijini Arusha, ambapo vyuo hivyo vilikubaliana kushirikiana katika kukabiliana na changamoto zinazoikumba nchi zao.

Alisema dhamira ya vyuo vyote ni kuhakikisha kuwa muunganiko huo unakua na kuwa chombo muhimu katika kushughulikia masuala muhimu ikiwemo matatizo ya maji, tabianchi, na afya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHILIP JACOB RUSHEMEZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 676 BNM** - Toyota Coaster yenye chassis namba **JT743P85108002103**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/142623/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LIVYO RAPHAEL MTEI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T 975 BJA AINA YA TOYOTA PRADO RANGI YA KIJANI FEDHA , KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/17428/2024.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**IDDY OMARY RAMADHAN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA TAE 563551 ILIYOTOLEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUPITIA MAMLAKA YA UHAMIAJI YA NCHI KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA HATI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/17444/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AZINAEL KOSHUMA** ZAWADIEL ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 845 ACG AINA YA TOYO YENYE JINA LA UMILIKI WA LIBERTY SAMSON KALAMJI. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHE POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SIM/BUS/4805/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ATHUMANI JUMA OMARI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 287 BKP - TOYOTA SPRINTER. CHASSIS NAMBA AE1100101948. ENGINE NAMBA 5AG782041. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/TAN/MUH/12102/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIANA GEOFREY MNZAVA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1874-0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MWANGA TRC CENTRE** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIL/MWA/25200/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LUSEKELO JAIRO MWANGYOMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 744 DGG. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/29273/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...79/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ZAKIR HASHIM wa MTAA WA SALUM ABDALLAH**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA NASRIN MAJID MOHAMED**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 8 mwezi 11 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...80/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HASHIM HAJI NOORMOHAMED wa MTAA WA SALUM ABDALLAH**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA MAJID MOHAMED ADAM**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 08 mwezi 11 mwaka 2024

..............................................
**HAKIMU**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27951 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE REV RAYMOND STANSLAUS KIPINGU**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY RAPHAEL MICHAEL KIPINGU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10TH day of December, 2024.

Dated at KOROGWE this 6TH day of November, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**MADAI NAMBA 8809/2024**
**Shauri ya Madai Namba 8809/2024**
**Katika Mahakama ya wilaya ya DODOMA**
**VICTORIA COSMAS MBELE.........MRUFANI**
**DHIDI YA**
**RAMADHANI ALLY KASALAMBA YAP MARKEZ .......MRUFANIWA**

**Kwa: RAMADHANI ALLY KASALAMBA**

Kwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya Alhamisi tarehe 14/11 Mwaka 2024. Unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakam hii leo.

Tarehe 08 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHARLES DESIDERI HOTAY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 855 DWF - NISSAN DUALIS. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHE POLISI. CONTROL **NUMBER 9910842747648**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**Telegramu: UHAMIAJI**
**Simu : 027-2751557**
**027-2752284**
**E-mail:riokilimanjaro@immigration.go.tz**
**KILIMANJARO**

**OFISI YA UHAMIAJI MKOA ,**
**S.L.P 1049,**
**MOSHI**

**Kumb. Na. IMM/MS/DN/163** **Tarehe 07/11/2024**



**HII NI TAARIFA KUWA:**
**YUSRA MOHAMED SAEED MIRZA -BOX 471MOSHI KILIMANJARO**

Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia wa Tanzania kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi .Yeye ni raia wa INDIA na Nchi atokayo ni INDIA .

Kazi yake /Shughuli zake ni Mwanafunzi, Anuani ya mwajiri wake/Shughuli zake ni BOX 471 MOSHI KILIMANJARO

Ameishi nchini tangu 2005, Pia amewahi kuishi Mkoa/ Mikoa ya hakuna, Mtu yeyeto mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

**Kamishna Jenerali wa Uhamiaji,,**
**S.L.P 512,**
**DAR ES SALAAM.**

**KNY: AFISA UHAMIAJI MKOA,**
**KILIMANJARO**

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**CIVIL CASE NO.26907 OF 2024**
**MOHAMMED INTERPRISES (TANZANIA) LIMITED--PLAINTIF**
**VERSUS**
**BOAZ ANYITIKE KYANDO---------- DEFENDANT**
**TO: BOAZ ANYITIKE KYANDO OF DAR ES SALAAM.**

**TAKE NOTECE** that hearing of the above suit has been set down for Mention on 13 day of 11, 2024 at 08:30am in forenoon thereafter at district court

You must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the document upon which you inted really in support of your case

Given under my hand and the seal of this 07th day of November,2024.

------------------
**DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE I/C**
**KYELA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELLY SHADRICK NJULUMI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 857 ATH aina ya LANDROVER DEFENDER 110 yenye jina la umiliki wa CHURCH OF CHRIST MISSION. Chassis namba: SALLDHMF71A972805. Engine namba: 16L28639A. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/43172/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BENSON DENIS MATULA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC208DHW aina ya TVS STAR. Chassis No. MD625AE31MTH00799, Engine No. BE3HM1700541. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/51080/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 264 LA 2023**
**MICHAEL ALOIS HAULE MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ASTERIA LEIYA MOSHI MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**ASTERIA LEIYA MOSHI**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**MICHAEL ALOIS HAULE** Amefungua shauri mbele ya baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala) Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe **18/11/2024 Saa 3:00Asubuhi** mbele ya **Mh. J.W. SILLAS.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 30 mwezi 09 mwaka 2024

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**BONAVENTURE EVARIST THOMAS,** MKAZI WA DAR ES SALAAM. AMEPOTEZA HATI YA KUSAFIRIA (PASSPORT) NAMBA **TAE407346** ILIYOTOLEWA NA IDARA YA UHAMIAJI MAKAO MAKUU. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI RB NO. **PHQ/DAR/ILA/246902/2024**

**FORM 58**
**IN THE DISRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28065 OF 2024 In the Matter of teh Estat5e of the Late FLORA KARUMBA RUGE**
**And**
**In the Matter of Application for lettres of administration by JAMES RUGE SANGI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate aof the above -named deceased arte hereby cited to come and see the poceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration ) is made to the abobe named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 08 day of 01 2025

Dated at DAR ES SALAAM this 08 day of 11 2024.

Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA.18956 YA 2024**
**MARTHA JUMA MTOGO............MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**FRANK BANDAGAMA YOHANA......MJIBU RUFAA**
**ALBERT MSHANGA......MJIBU RUFAA**

**KWA: ALBERT MSHANGA**
**POPOTE PALE ALIPO.**
**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA.18956 YA MWAKA 2024 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu liltatajwa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE.E.E KAKOLAKI,JAJI wa Mahakama kuu Tanzania Dodoma,saa tatu (3:10) asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 14/11/2024.

HIVYO;Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

NA ENDAPO; Hutafika wewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.

IMETOLEWA ;Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 16/10/2024

..................................................
**NAIBU MSAJILI**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Ishiba ateuliwa kuwa Waziri Mkuu Japan

**TOKYO,** Japan

BUNGE la nchini Japan limepiga kura na kumchagua Shigeru Ishiba (pichani chini) kuhudumu katika nafasi ya waziri mkuu ambaye ataongoza serikali ya wachache baada ya chama chake kupata hasara kubwa katika uchaguzi uliofanyika mwezi uliopita.

Licha ya kukiongoza chama chake kwa hasara kubwa katika uchaguzi mkuu mwezi uliopita, Waziri Mkuu wa Japan Ishiba, alishinda kura katika Bunge jana na kufanikiwa kuendelea kuwa kiongozi wa nchi hiyo.

Ilielezwa kuwa kiongozi huyo ambaye Chama chake cha 'Liberal Democratic' kilipoteza wingi wake wa wabunge kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 15 mwezi uliopita, ataongoza vyema serikali ya wachache.

Matokeo hayo yanamweka Ishiba katika hali ya hatari huku serikali yake ikiendelea kukabiliana na kashfa ya fedha za kisiasa, pamoja na mfumuko wa bei, uhaba wa wafanyakazi na mizigo inayoongezeka ya wazee.

Wachambuzi walisema Ishiba anaweza kuhangaika kuendelea kuishi kwa muda mrefu, jambo linaloiweka Japan katika hatari ya kurejea kwenye mlango unaozunguka wa mawaziri wakuu wakati tu inapojiandaa kukabiliana na hali ya kutotabirika nchini Marekani, ambaye ni mshirika wake muhimu zaidi wa kimataifa, baada ya kuchaguliwa kwa Donald Trump kama rais.

Katika uchaguzi wa marudio na kiongozi wa chama cha 'Constitutional Democratic Party', ambalo linatajwa kama kundi kubwa la upinzani nchini humo, Ishiba alimshinda Yoshihiko Noda, waziri mkuu wa zamani, kwa kura 221 dhidi ya 160.

Ingawa Wanademokrasia wa kikatiba walipata mafanikio makubwa katika uchaguzi wa mwezi uliopita, hawakupata wingi wa kura katika Bunge, jambo ambalo lingewapa haki ya kuchagua waziri mkuu. Pamoja na vyama vingine saba vidogo vya upinzani kusimamisha wagombea, na kwamba Noda hakuweza kukusanya uungwaji mkono wa kutosha kumng'oa Ishiba.



**NEW YORK TIMES**

# Rais Biden, Trump, Putin kujadili vita vya Ukraine

• Donald Trump aanza kupanga safu



Tom Homan (62) kulia, na Elise Stefanik (40) miongoni mwa maofisa walioteuliwa na Rais Mteule wa Marekani Donald Trump, kuhudumia katika nafasi ya ukuu wa mipaka na balozi katika Umoja wa Mataifa (UN). **PICHA: MTANDAO**

**Na Maulid Mmbaga**

IKULU ya White House imesema Rais wa Marekani Joe Biden amemualika Rais mteule Donald Trump ofisini kwake Jumatano ili kujadiliana kuhusu vipaumbele vya sera za ndani na nje, na kwamba vita vya Ukraine ni miongoni mwa mambo yatakayojadiliwa.

Aidha, kwa mujibu wa Gazeti la 'Washington Post' Rais Mteule Trump alimsisitiza mwenzake wa Russia Vladimir Putin kutoendelea kuchochea vita nchini Ukraine, katika mazungumzo kwa njia ya simu waliyoyafanya Alhamisi.

Mshauri wa masuala ya Usalama wa Marekani, Jake Sullivan, alisema jana kwamba Rais Biden anatarajiwa pia kutoa wito kwa Trump kutoiacha Ukraine.

Kwenye mahojiano na kituo cha utangazaji cha CBS, Sullivan alisema ujumbe muhimu wa Biden utajikita katika makabidhiano ya amani ya madaraka, lakini pia atamweleza Trump kile kinachoendelea barani Ulaya, Asia na Mashariki ya Kati.

"Rais atakuwa na nafasi ya kumueleza Rais mteule Trump juu ya namna anavyoyaangazia mambo, msimamo wake na namna Trump atakavyoshughulikia masuala hayo atakapoingia madarakani," alisema Sullivan.

Ingawa Sullivan hakufafanua kwa kina ni maeneo gani hasa yatagusiwa, lakini huenda wakajikita kwenye vita vya Russia na Ukraine, ambavyo Trump ameahidi kuvimaliza mara moja, ingawa bado hajasema ni kwa namna gani, licha ya kwamba Marekani imekuwa mfadhili mkubwa wa Ukraine.

Ilielezwa kuwa Washington tayari imetoa msaada wa mabilioni ya dola kuisaidia Ukraine kijeshi na kiuchumi, tangu ilipovamiwa na Russia, Februari 2022, lakini mara kwa mara Trump amekuwa akikosoa hatua hiyo.

Kadhalika, ilielezwa kuwa ili kuiweka Ukraine katika nafasi imara zaidi kwenye uwanja wa vita na kuwa katika nafasi yenye nguvu zaidi kwenye meza ya mazungumzo, utawala wa Biden unapanga kutumia dola bilioni sita zilizosalia kabla ya kuwasili kwa Donald Trump madarakani.

Sullivan anatoa matamshi hayo wakati Ukraine ikiishambulia Moscow Jumapili kwa droni karibu 34, hilo likiwa ni shambulizi kubwa kabisa la droni kwenye mji mkuu wa Russia tangu kuanza kwa vita hivyo.

Hata hivyo, gazeti hilo la Washington Post, lilinukuu vyanzo viwili vyenye uelewa na mazungumzo hayo ambao hawakutaka kutambulishwa kwamba Trump alimkumbusha Putin juu ya ukubwa wa jeshi la Marekani barani Ulaya, na kwamba alielezea nia ya mazungumzo ya zaidi kuhusu suluhisho la vita vya Ukraine hivi karibuni.

Vile vile, Rassia ilibainisha kwamba Rais Mteule wa Marekani alikuwa ametuma ishara chanya wakati wa kampeni kuhusu mzozo huo, kwakuwa alizungumzia uwezekano wa amani na hakuonyesha nia ya kuisababishia nchi hiyo ushindi wa kimkakati.

### EU RUSSIA IWAJIBIKE

Katika hatua nyingine, Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya (EU) Josep Borrell alisema kwamba Russia itatakiwa kushitakiwa kwa makosa ya uhalifu wa kivita iliyoyafanya nchini Ukraine, katika makubaliano yoyote ya amani ya siku za usoni, pamoja na kulipia uharibifu iliousababisha.

Borrell alisema ili suala la amani litekelezwe kwa uhalisia inatakiwa kuwa ya haki na endelevu, akisisitiza kwamba jambo la muhimu vita hivyo vinatakiwa kumalizwa kwa namna ambayo kutakuwa na kuwajibika sio tu kiuchumi na haki, lakini pia masuala yatakayosaidia amani ya kudumu.

Trump anatarajiwa kuingia madarakani Januari 20, 2025 baada ya kumuangusha Makamu wa Rais Kamala Harris kwenye uchaguzi wa Novemba 5, mwaka huu.

### UTEUZI

Katika uamuzi wake wa kwanza kuhusu wafanyakazi, Trump amemteua meneja wa kampeni Susie Wiles mwenye ushawishi mkubwa anayesifiwa kusaidia kuhakikisha kurudi kwake White House kama mkuu wa wafanyakazi.

Kiongozi huyo pia alifanya uteuzi wa maofisa wawili akiwemo Tom Homan (62), atakaehudumu kama mkuu wa mipaka ili kutekeleza sera ya Trump ya kuzuia wahamiaji haramu kuingia nchini humo na hapo awali aliwahi kuwa kaimu mkurugenzi wa Uhamiaji na Forodha (ICE).

Mwingine ni Mbunge wa New York Elise Stefanik (40), atakaehudumu kama balozi katika Umoja wa Mataifa (UN).

Wakati huo huo, Chama cha Republican cha Trump kinakaribia kudhibiti kikamilifu Bunge la Marekani, na kwamba tayari wanathibiti Seneti na wanahitaji kushinda viti vichache tu ili kuchukua Bunge la Wawakilishi.

Kwa mujibu wa vyanzo vya kuaminika chama hicho kinahitaji viti 218 ili kushinda wingi wa Wabunge. Warepublican wana 215 ikilinganishwa na wapinzani 210 wa Democrats.

Ilielezwa kuwa udhibiti wa Bunge hukipa chama kilicho madarakani uwezo wa kuanzisha sheria nguvu ya kuanzisha kesi za kuwashtaki maofisa.

Aidha, ilielezwa kuwa matokeo ya mwisho yanayotokana na uchaguzi wa Novemba 5, yanaendelea kumiminika, na Warepublican wakishinda katika Seneti huku udhibiti wa Baraza la Wawakilishi ukiwa bado haujabainishwa.

Pia Rais Biden, akihutubia taifa kwa mara ya kwanza tangu ushindi wa Trump, alimshukuru Kamala Harris kwa kampeni ya kusisimua na kuahidi uhamisho wa amani na utaratibu wa mamlaka. **Chanzo Mitandao**

HABARI MICHEZO

# AHOUA, FEI TOTO, KIHIMBWA WACHUANA 'ASISTI' LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mpya wa Simba raia wa Ivory Coast, Jean Charles Ahoua na viungo wawili Watanzania, Feisal Salum wa Azam FC na Salum Kihimbwa wa Fountain Gate, wanaongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia raundi ya 10.

Kwa mujibu wa takwimu zetu pamoja za Bodi ya Ligi, wachezaji wote hao wana 'asisti' nne kila mmoja.

Hata hivyo, Ahoua anakaa juu yao kutokana na kufunga mabao matano mpaka sasa kwenye ligi, akiwa amehusika na mabao tisa kwenye timu yake ya Simba.

**Kiungo huyo anayeshika nafasi ya pili kwenye ufungaji bora wa ligi mpaka sasa, alisajiliwa msimu huu kutoka klabu ya Stella Adjame ya nchini kwao.**

Kihimbwa ana 'asisti' nne, akiwa amepachika mabao matatu mpaka sasa, hivyo akihusika na mabao saba mpaka sasa, huku 'Fei Toto' akiwa na 'asisti' nne, akifunga bao moja, akihusika na mabao matano kwenye kikosi cha Azam FC.

Viungo hao watatu, wanafuatiwa na kiungo mwingine wa Yanga, raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, ambaye ana 'asisti' tatu mpaka sasa, akiwa amefunga bao moja pamoja na Ande Koffi wa Singida Black Stars ambaye yeye hajafunga bao lolote.

Kwa upande wa mabao, anayeongoza ni Selemani Mwalimu wa Fountain Gate akifikisha mabao sita hadi kufikia raundi ya 10, Ahoua wa Simba akishika nafasi ya pili akiwa na mabao matano, Edgar William wa Fountain Gate na Peter Lwasa wa Kagera Sugar, wenye mabao manne kila mmoja.

Wanaoshika nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji kwenye Ligi Kuu, wana mabao matatu kila mmoja ambao ni Joshua Ibrahim wa KenGold, Maxi Nzengeli wa Yanga, Elvis Rupia na Marouf Tchakei wote wa Singida Black Stars, Offen Chikola wa Tabora United, Nassor Saadun wa Azam FC, Paul Peter wa Dodoma Jiji, Maabad Maulid wa Coastal Union, na Kihimbwa wa Fountain Gate.

SOKA...



Vijana wa kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Kituo hicho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Singida yatoa sababu Adebayor kutoonekana*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Black Stars, imesema mchezaji wao Victorien Adebayor raia wa Niger hajaonekana kwenye kikosi hicho kwa sababu za kiufundi, lakini yupo nchini akiendelea na mazoezi na wenzake kama kawaida.

Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Jonathan Kassano, ametoa ufafanuzi huo kutokana na mashabiki wa soka kushangazwa na kutoonekana kwa mchezaji huyo uwanjani huku akiwa amesajiliwa na timu hiyo kama mmoja wa mastaa wa kikosi hicho.

Kassano alisema kucheza au kutocheza kwa mchezaji huyo kunatokana na mwalimu mwenyewe na wao kama viongozi hawawezi kumpangia kikosi Kocha Mkuu, Patrick Aussems ambaye ameifanya timu hiyo iwe kwenye kiwango bora kwa sasa.

"Adebayor yupo suala anacheza lini inabaki kwa mwalimu, maana kwa sasa kuna mechi za Ligi Kuu tu, mwalimu nadhani anaendelea kuwatumia wachezaji ambao alianza nao 'pre season', ameendelea kuwatumia hao hadi pale atakapoamua kuwatumia, yupo, ni mchezaji wetu na anaendelea kufanya mazoezi na kikosi,"alisema Mtendaji Mkuu huyo.

Mchezaji huyo alikuwa gumzo mwaka 2022, wakati akiichezea klabu ya USGN ya Niger alipofanya vizuri kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, kiasi cha kuivutia Simba iliyokuwa nao kundi moja na ilikuwa karibu atue Msimbazi, lakini RS Berkane ya Morocco ilishinda vita hiyo na kumsajili.

Hata hivyo, tetesi za kutaka kutua Msimbazi zilizuka tena, lakini akatua AmaZulu FC ya Afrika Kusini kwa muda mfupi, kabla ya kwenda AS Singida na sasa Singida Black Stars.

Kassano alisema kwa sasa kikosi hicho kimerejea kambini kujiandaa na michezo inayofuata ya Ligi Kuu.

"Baada ya michezo yetu miwili tuliocheza Zanzibar, mwalimu alitoa mapumziko wa siku tatu, kikosi tayari kimerejea mazoezini wapo kambini Singida, wanaendelea kuandaliwa kwa ajili ya michezo inayofuata ya Ligi Kuu," alisema.

Timu hiyo inashika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 23 baada ya kucheza michezo 10, ikishinda mechi nane, sare moja na kupoteza mchezo mmoja.

## KMKM haikuwa na malengo ya suluhu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM SC imesema sare waliyoipata katika mchezo wao dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga haikuwa katika mipango yao.

Juzi Jumapili KMKM SC ilijikuta ikitoa salute kwa maafande wenzao wa Kipanga FC kwa kulazimisha suluhu kwenye mchezo uliochezwa katika uwanja wa Mau.

Akizungumza na Nipashe masra baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Kocha wa timu hiyo, Ame Msimu alisema walishuka uwanjani kwa malengo ya kupata alama tatu baada ya kushindwa kupata alama hizo katika mchezo wao uliopita.

Alisema alitegemea kuona wachezaji wake wanajituma ili kufanikisha lengo lao lakini mambo yalikuwa tofauti kutokana na ushindani walionesha wapinzani wao.

Alisema kwa ujumla mchezo huo ulikuwa mgumu kwakuwa wapinzani wao walijua kuzisoma mbinu zao ndani ya mchezo.

Alisema wachezaji wake walicheza vizuri katika muda wote wa mchezo licha ya makosa kadhaa yaliyojitokeza katika mchezo huo.

Alisema walikosa umakini lakini pia kutambua mbinu za wapinzani wao mchezoni hali iliyopelekea kushindwa kutumia nafasi wanazopata.

"Tulicheza vizuri, licha ya mchezo kuwa mgumu kwa pande zote, tulitengeneza nafasi chache za wazi lakini tulikosa umakini katika kuzitumia nafasi hizo," alisema.

Kwa Matokeo hayo KMKM SC imefikisha pointi 16 na kubakia nafasi yake ya saba huku Kipanga FC wakifikisha ponti 14 na kujiweka nafasi ya tisa katika msimamo Ligi.




**Tulicheza vizuri, licha ya mchezo kuwa mgumu kwa pande zote, tulitengeneza nafasi chache za wazi lakini tulikosa umakini katika kuzitumia nafasi hizo.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### YAKOMAA NA ZUBIMENDI

KLABU ya Manchester City iko tayari kulipa euro milioni 60 kama kipengele cha kumuachilia kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, huku wakiendelea kutafuta mbadala wa Mhispania mwenzake Rodri Januari. ***(mirror)***

### VALVERDE PIA AWINDWA

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Federico Valverde mwenye umri wa miaka 26, ni mchezaji mwingine anayewaniwa na Manchester City, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay ana kipengele cha kuachiliwa cha euro bilioni moja. ***(Fichajes)***

### HAALAND ANAFIKIRIA PSG

PARIS St-Germain ni mpango B kwa fowadi wa Manchester City, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 24, huku Barcelona na Real Madrid pia zikimtaka raia huyo wa Norway, ambaye mkataba wake unamalizika 2027. ***(Soka365)***

### NKUNKU ATAKIWA MAN

MANCHESTER United inataka kumnunua mshambuliaji wa Chelsea, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 26, kwani Mfaransa huyo hajafurahishwa na muda wake wa kucheza chini ya Enzo Maresca. ***(L'Equipe via Express)***

### TAH ANYATIWA NA VIGOGO

KLABU ya Manchester United pia imeungana na Barcelona katika mbio za kuwania kumnunua mlinzi wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 28. ***(Fichajes)***

### WATAKIWA REAL MADRID

MLINZI wa kati wa Tottenham Hotspur na Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 26, na mlinzi wa Everton, Jarrad Branthwaite mwenye miaka 22, wametambuliwa na Real Madrid kama wachezaji wanaoweza kuwasajili. ***(Caught Offside)***

### ZAMTAKA WATURU ENDO

KIUNGO wa kati wa Liverpool, Wataru Endo mwenye umri wa miaka 31, anahitajika sana huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Japan akiendelea kutatizika huko Anfield. AC Milan, Fulham, Wolves na Ipswich zote zina nia ya kumsajili. ***(Caught Offside)***

### BUONANOTTE KUTUA SPURS

TOTTENHMA Hotspur inatamani kumnunua kiungo wa kati wa Argentina, Facundo Buonanotte mwenye umri wa miaka 19, lakini italazimika kushindana na Leicester City. ***(Fichajes)***

### KURUDI SANTOS UHAKIKA

MKURUGENZI wa Santos, Marcio Calves amesema kurejea kwa Neymar mwenye umri wa miaka 32, katika klabu yake ya zamani itakuwa "ndoto ya kila shabiki" na ingawa hakuna "mazungumzo rasmi" yaliyofanyika na klabu yake ya sasa ya Al-Hilal, lakini ana uhakika wa asilimia 60 kwamba mshambuliaji huyo wa Brazil atakamilisha uhamisho mkataba wake utakapokamilika Juni. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# ARTETA AHOFIA MAJERUHI ARSENAL

**LONDON,** England

**Kocha huyo ametilia shaka upatikanaji wa Bukayo Saka na....**

MIKEL Arteta amesema anaiombea Arsenal kuepuka kupata na majeruhi zaidi wakati huu wa mapumziko ya mechi za kimataifa.

**Kocha huyo wa Arsenal alitilia shaka upatikanaji wa Bukayo Saka na Declan Rice kwa mechi za Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Ugiriki na Jamhuri ya Ireland wiki ijayo baada ya wawili hao kushindwa kumaliza mchezo kwenye sare ya 1-1 ya Jumapili ya Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea.**

Rice alianza licha ya kuvunjika kidole cha mguu wiki moja iliyopita huko Newcastle huku Saka akichechemea dakika tisa kabla ya mchezo kumalizika uwanjani Stamford Bridge kwa tatizo ambalo halijabainishwa.

Martin Odegaard alianza mchezo wake wa kwanza kwa Arsenal tangu Agosti 31 baada ya kupata jeraha la kifundo cha mguu akiwa kwenye majukumu ya kimataifa na Norway, huku Gabriel Martinelli akiuguza maumivu ya mguu alipokuwa na Brazil mwezi uliopita.

Arsenal imekuwa bila Jurriën Timber, Thomas Partey, Ben White na Takehiro Tomiyasu msimu huu na hawatacheza tena hadi watakapowakaribisha Nottingham Forest kwenye Uwanja wa Emirates Novemba 23 mwaka huu.

Arteta alisema: "Ninachoomba ni kwamba baada ya mapumziko ya kimataifa tuwe na timu ikiwa imejipanga kikamilifu. Wawepo na wako fiti.

"Shaka baada ya shaka, suala baada ya suala, si tu kwa wale ambao hawana uwezo wa kucheza, lakini na wale ambao wanaweza kucheza kwa muda fulani tu na wasio na uwezo wa kucheza."

Alipoulizwa hasa iwapo Saka na Rice wataweza kuichezea England, Arteta alijibu:

"Haionekani vizuri, kwa sababu kwa wachezaji wawili wenye umuhimu huo kukuambia hawawezi kuendelea na mchezo, ni wazi kwamba si habari njema.

"Ni wachezaji wawili ambao wametoka majeruhi hivi karibuni, sijui nitegemee watakuwa fiti," alisema.

Arteta pia anapanga kuzungumza na Ødegaard kabla ya kuamua iwapo atajiunga na Norway mwezi huu.

# FLICK ALIA LEWANDOWSKI KUNYIMWA BAO




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick alikosoa "uamuzi mbaya" wa kukataa bao la Robert Lewandowski lililoonekana kwamba ameotea wakati timu yake ikichapwa 1-0 na Real Sociedad Jumapili kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Lewandowski alifunga bao dakika ya 14, lakini teknolojia ya kuotea ya nusu-otomatiki (SAOT), iliyoanzishwa nchini Hispania mwanzoni mwa msimu, iliamua kwamba mguu wa mshambuliaji huyo ulikuwa mbele ya mguu wa beki wa Nayef Aguerd.

Wenyeji walipata bao pekee na la ushindi katika mchezo huo kupitia kwa mkwaju wa Sheraldo Becker, na hivyo kuhitimisha mfululizo wa ushindi wa Barca katika michezo saba mfululizo katika mashindano yote, huku timu hiyo ya Flick ikishindwa kupata bao kwenye mchezo kwa mara ya kwanza msimu huu.

"Ulikuwa uamuzi mbaya," alisema Flick akiiambia Barça One baada ya mechi.


"Niliona picha hiyo, iko wazi, lakini lazima tuikubali. Halikuwa kosa la mwamuzi. Mwisho wa siku sisi ni binadamu, tunafanya makosa, na leo (juzi) lilikuwa kosa kubwa."

SAOT haitumiki Ulaya kote, ligi kuu ya Italia, Serie A, ilikuwa ligi kuu ya kwanza kuitumia na kuna nia ya kuianzisha kwenye Ligi Kuu ya England. Flick alisisitiza kwamba Lewandowski alikuwa katika sehemu sahihi wakati akifunga bao hilo.

"Sina hasira sana, lakini inaumiza," alisema.

"Nilimwambia tu 'Lilikuwa goli, ulikuwa uamuzi mbaya, haukuotea.'

Kipigo cha pili cha Barca katika ligi msimu huu pia kilikuja huku Lamine Yamal akitazama mchezo akiwa jukwaani baada ya kuumia kifundo cha mguu wakati wa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki dhidi ya Red Star Belgrade.



# Maresca: Chelsea ipo kwenye mbio za ubingwa

**LONDON,** England

ENZO Maresca amesisitiza kuwa Chelsea ipo kwenye hatua ya kumshinda mmoja wa wapinzani wao katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya timu yake kutoka sare ya 1-1 na Arsenal Uwanja wa Stamford Bridge Jumapili.

Chelsea ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi, na bao la Pedro Neto dakika ya 70 liliwawezesha kupata pointi moja dhidi ya Arsenal baada ya Gabriel Martinelli kuwafungia washikabunduki dakika ya 60.

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa Chelsea bado inasubiri kupata ushindi katika ligi chini ya Maresca baada ya kufungwa na Manchester City na Liverpool.

Lakini baada ya sare hiyo, Maresca ana imani Chelsea hivi sasa ipo karibuni kupata ushindi mnono dhidi ya timu hizo zilizo kileleni kwenye msimamo.

"Nilisema mara nyingi, unafikiri tunastahili kupoteza kwa Liverpool? Hapana. Hivi karibuni tutashinda aina hizi za michezo.

"Lakini angalia dhidi ya Bournemouth ugenini hatukustahili kushinda, na tulifanya hivyo dhidi ya Crystal Palace na Nottingham Forest, tulistahili kushinda, na hatukuweza kushinda hivi karibuni.

Aliongeza: "Tuna furaha sana. Kwangu mimi tuko nyuma ya klabu za aina hii kama vile City na Arsenal.

"Tuko nyuma yao, lakini Chelsea ni moja ya klabu kubwa duniani na tunahitaji kushindana na kujaribu kushinda michezo inayokuja."

Chelsea ilimuanzisha Cole Palmer baada ya kupata jeraha dhidi ya Manchester United wikendi iliyopita baada ya kukabiliwa na changamoto kutoka kwa Lisandro Martínez.

# Vibali kumchelewesha Amorim kutua Man United

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim anakabiliwa na kucheleweshwa zaidi kabla ya kuanza rasmi kazi kama kocha mkuu mpya wa Manchester United, huku klabu ikisubiri uthibitisho wa visa yake, kwa mujibu wa ESPN.

Man United ilimtangaza Amorim kama kocha wao mpya Novemba Mosi mwaka huu.

Amorim mwenye umri wa miaka 39, jana Jumatatu alitarajiwa kuwasili jijini Manchester, lakini chanzo kiliiambia ESPN kuwa bado anasubiri kupata kibali rasmi cha kuanza kazi yake.

Hata hivyo, hadi uthibitisho utakapopokelewa, Amorim hawezi kuanza kazi zake rasmi, ikiwa ni pamoja na kusimamia vipindi vya mazoezi.

Wachezaji kadhaa hawatakuwepo pale kwenye uwanja wa mazoezi wa Carrington baada ya kujiunga na timu zao za taifa baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Leicester Uwanja wa Old Trafford Jumapili.

Wachezaji ambao hawajaitwa kwenye majukumu ya kimataifa wamepewa likizo.

Mechi ya kwanza ya Amorim kuiongoza Man United itakuwa dhidi ya Ipswich Town kwenye Uwanja wa Portman Road Novemba 24.

Kocha huyo wa Ureno atachukua mikoba ya Ruud van Nistelrooy ambaye amesimamia mechi nne bila kufungwa.

Muda wake uliisha kwa ushindi mzuri dhidi ya Leicester, na baadaye, alifichua kuwa bado anasubiri kusikia kama atakuwa sehemu ya benchi la Amorim.

"Nilifurahia mawasiliano ya wazi ya klabu, ulikuwa muda mfupi," alisema Van Nistelrooy.



## Bodi ya Ligi yaijadili Yanga kuhamia KMC

INATOKA UK. 24

kusikika kuwa viongozi walikuwa na mpango wa kutaka kuhama kwenye uwanja huo.

Juzi klabu hiyo ilitoa taarifa yake rasmi kupitia Ofisi ya Mtendaji Mkuu kuwa timu hiyo ikielezea kuhamia Uwanja wa KMC.

Hata hivyo uwanja huo kwa sasa unatumiwa na timu ya Simba na KMC kama viwanja vya nyumbani hivyo kama Yanga itakubaliwa, basi ni wazi kuwa ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara itabadilika, hasa tarehe ambazo timu hizo zilitakiwa kucheza kwa siku moja kwenye viwanja vya nyumbani.

## Simba yaongoza Ligi Kuu na rekodi kibao

INATOKA UK. 24

akisisitiza kuwa bado hakijafika sehemu ambayo anataka.

"Nadhani hapa iko kwenye asilimia 55 tu, kuna kitu ambacho nakihitaji sijakiona. Kuna vitu vingine tumefanya vizuri, ikiwemo baadhi ya wachezaji kuanza kujiamini, timu imeanza kuwa na muunganiko mzuri, wameanza kuelewana, mmoja akiwa na mpira wanajua mwenzake anaweza kuwa wapi, mikimbio yake ni ipi, anakwenda kasi au taratibu, hili tumeshafanikiwa, nilikuwa pia nataka wachezaji wanaobaki benchi nao wawe msaada kwenye timu, nimeanza kuona, lakini kiufundi kuna vitu havijakaa sawa, ikiwemo kasi kwa dakika zote 90, kikikaa mabadiliko yataonekana." alisema Fadlu raia wa Afrika Kusini.

Kikosi cha Simba kwa sasa kimerejea mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis unaitarajiwa kuchezwa Novemba 27, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.



# MKONGWE YANGA ASHANGAA WACHEZAJI KUCHEZA 'KIFAZA'

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa zamani wa Yanga, Makumbi Juma, amesema moja ya sababu ambayo imeifanya timu hiyo kupoteza michezo miwili mfululizo katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ni kucheza 'kifaza' kwa siku za karibuni, tofauti ya ilivyozoeleka huko nyuma.

Makumbi, ambaye alitisha kwa kupachika mabao akiwa na timu hiyo pamoja na timu ya taifa ya Tanzania kiasi cha mashabiki wa Yanga kumpachika jina la 'Homa ya Jiji', alisema msimu huu wachezaji wa timu hiyo wamebadilika na hawachezi kwa kujituma tena huku wakionekana kuridhika na mafanikio waliyoyapata huko nyuma.

"Nilichokigundua kwa siku za karibuni wachezaji wetu wanacheza kistaa sana, wanacheza 'kifaza', maana yake wao tayari ni wakubwa, wamekuwa maarufu, hivyo hawajitumi tena kwa sababu kila mmoja anafahamu wao ni nani, hiki kitu si kizuri, wabadilike," alisema Makumbi.

**Aliwataka viongozi wa timu hiyo haraka wakae na Kocha Mkuu Miguel Gamondi ili awaambie wachezaji kuhusu mabadiliko ya uchezaji katika kikosi chao.**

"Ningependa viongozi wakae na mwalimu awaambie kuhusu uchezaji wao na nidhamu yao. Siku hizi Yanga ikicheza na timu ambayo ina kasi, wanapambana na wana fiziki vizuri basi mechi kwao inakuwa ngumu sana tofauti na misimu miwili iliyopita, umeona mechi dhidi ya Tabora United na hata Singida Black Stars japo tulishinda bao 1-0," alisema.

Straika huyo mkongwe aliwataka viongozi wa klabu hiyo kuacha mpango wa kumtimua kocha Gamondi kama upo kwani haoni kama yeye ni sababu, badala yake kuna mambo kidogo tu ya kubadilika. "Sidhani kama ni sahihi kumtimua kocha kwa kufungwa, timu nyingi zinafungwa na hakuna timu isiyofungwa duniani," alisema.

Kuhusu kocha huyo kupenda kutumia wachezaji hao hao badala ya kubadilisha kitu ambacho kimemfanya kulaumiwa na baadhi ya wachambuzi, Makumbi alisema inawezekana kuna wachezaji wana mikataba migumu inayowataka kucheza kila mechi.

"Wachezaji wa sasa tofauti na sisi wa zamani, wanalipwa pesa nyingi na mikataba ina vipengele vingi, kuna baadhi wanaweza kuweka kipengele cha kucheza kila mechi ndiyo maana unaona kila mechi wapo, wengine ikitokea penalti anapiga yeye, imo kwenye mkataba, inawezekana kabisa kosa siyo la kocha, ni mikataba ya wachezaji," alisema.

Tangu kupoteza mechi mbili mfululizi, ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC na mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, hali imekuwa si tulivu sana kwenye klabu ya Yanga huku baadhi wakimnyooshea kidole Gamondi, lakini wengine lawama wakizitupa kwa baadhi ya wachezaji wa timu hiyo kwa kile kinachodaiwa kushuka viwango.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kushoto) akicheza muziki katika Kongamano la Wajasiriamali lililofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tchakei afurahia tuzo mchezaji bora Oktoba*

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Singida Black Stars, Marouf Tchakei, amesema tuzo ya mchezaji bora wa mwezi Oktoba ni chachu kwake ya kuendelea kufanya vizuri kwenye kikosi cha timu yake.

Nyota huyo raia wa Togo wiki iliyopita alitangazwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu kwa mwezi Oktoba pamoja na kocha wa Azam FC, Rachid Toussi aliyetangazwa kuwa kocha bora.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Tchakei alisema tuzo hiyo imempa hamasa ya kuendelea kujituma kwenye timu yake na kusaidia kufanya vizuri.

"nawashukuru wachezaji wenzangu kwa ushirikiano wao.., hii tuzo ni chachu ya kuendelea kufanya vizuri na kusaidia timu kufanya vizuri zaidi," alisema nyota huyo.

Alisema ligi ni ngumu na yenye ushindani hivyo lazima kama wachezaji wajitume katika kila mchezo kuweza kupata ushindi utakaoisaidia timu hiyo kuendelea kukaa kwenye nafasi za juu.

Singida Blac Stars inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 23 baada ya kucheza michezo 10 ikizidiwa kwa pointi mbili na vinara wa Ligi hiyo, Simba huku Yanga ikiwa kwenye nafasi ya pili na pointi 24.


# Michezo

Jumanne Novemba 12, 2024

Nipashe




Arteta ahofia majeruhi UKURASA 21



Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (aliyeruka juu) akimtoka beki wa Leicester City, Wout Faes katika mchezo wa Ligi Kuu ya England juzi kwenye uwanja wa Old Traford, United ilishinda mabao 3-0. **PICHA: REUTERS**

# Simba yaongoza Ligi Kuu na rekodi kibao

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Ndio timu iliyofunga mabao mengi zaidi huku pia ikiwa na rekodi ya...

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imesimama kupisha michezo ya timu za taifa huku ikiongoza kwenye msimamo kwa kuwa na pointi 25, Simba ina rekodi nyingine nyingi za kuvutia mpaka sasa.

**Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Simba imefunga mabao 21 na kuwa timu pekee iliyopachika mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.**

Simba pia ina rekodi ya kukusanya pointi nyingi ikiwa nyumbani kuliko timu nyingine yoyote ambapo kati ya pointi 25 ilizonazo, 13 imezipata ikicheza michezo ya nyumbani.

Timu hiyo imecheza mechi sita ikiwa nyumbani na kufanikiwa kushinda mechi nne, imetoka sare na kupoteza mchezo mmoja.

Simba ilianza Ligi kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United, ikapata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Fountain Gate, ikazifunga Namungo FC mabao 3-0, KMC mabao 4-0, huku ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union na kupoteza kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Takwimu zinaonyesha imefunga mabao mengi kuliko timu yoyote ikicheza nyumbani, ikiwa imepachika mabao 16.

Timu hiyo imecheza mechi nne tu ugenini ambapo imeshinda zote na kukusanya pointi 12.

Michezo minne ambayo imecheza ikiwa ugenini ni dhidi ya Azam FC ikishinda mabao 2-0, ikazifunga Dodoma Jiji bao 1-0, Mashujaa FC 1-0 na Prisons 1-0.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, alisema mpaka wanakwenda mapumziko ameridhishwa kwa kiwango cha wachezaji wake, lakini

INAENDELEA UKURASA 23

# Bodi ya Ligi yaijadili Yanga kuhamia KMC

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi imesema imepokea barua ya klabu ya Yanga inayoomba kuhama kutoka, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, na kuhamia, KMC Complex kwa sasa wapo kwenye mchakato na kutazama sababu pamoja na kanuni ili kutoa uamuzi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema kuwa barua hiyo ilipokelewa juzi na sasa iko kwenye mchakato na siku si nyingi watatoa maamuzi ya kuwakubalia ama vinginevyo.

Klabu ya Yanga juzi ilitangaza kuhama Uwanja wa Azam Complex na kuhamia KMC Complex, katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA ambalo bado halijaanza.

"Tumepokea barua ya Yanga kutaka kucheza Uwanja wa KMC Complex, nadhani leo (Jumatatu) siku ya kazi, vijana wataanza kazi ya kuichakata, baada ya hapo tutakuwa na nafasi nzuri na kutangaza maamuzi ya Bodi.

Barua inaeleza makusudio yao ya kuhama kutoka Uwanja wa azam Complex kwenda KMC Complex, Mwenge, wameeleza sababu zao lakini zinabaki kuwa siri yetu baina ya klabu na Bodi na wamiliki wa uwanja wa Azam,

Sababu zinafikirisha, zina mashiko au hazina mashiko, hayo yote yapo kwenye mchakato, sisi tunautazama mpira zaidi, Bodi ni chombo cha klabu zote kwa hiyo kipo kwa maslahi yao kama chombo chao, tunakaa kujiridhisha," alisema.

Hata hivyo alisema yote hayo ni lazima yawe kwenye kanuni, hivyo pia watakaza kanuni zinasemaje, lakini bila kuacha maslahi ya kimpira.

Baada ya kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United Alhamisi iliyopita kwenye uwanja huo ikiwa ni siku chache tu tangu kupokea kipigo kingine cha bao 1-0 dhidi ya Azam FC, tetesi zilianza

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >